# Haja ya Imamu

Na
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

# Haja ya Imamu

Tafsiri ya Kiswahili ya: Dharuratul-Imam (Urdu)

Na: **Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi**

**Mfasiri:** Sheikh Yusufu Athuman Kambaulaya

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1897
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2018

**© Islam International Publications Ltd.**

**Kimeenezwa na:**
Islam International publications Ltd.
Unit 3, Bourne Mill Business Park
Guildford Road, Farnham, Surrey GU9 9PS, UK

*Kwa Maelezo Zaidi:*

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
Ahmadiyya Muslim Association
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +255222111031

**Kimechapwa na:**

ISBN: 978-1-84880-536-1
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# MAELEZO YA MWENEZI

## KUHUSU MWANDISHI

Mwandishi wa kitabu hiki, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Mau‘udi na Imam Mahdias, alizaliwa tarehe 13 Februari 1835 huko Qadian, India. Alijitolea maisha yake yote kujifunza elimu ya Kurani Tukufu na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Kwa kuona hali duni ya Waislamu na kushambuliwa sana na wapinzani, alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya mafanikio ya Islam. Vile vile alijitolea kujibu shutuma za wapinzani na kutetea dini ya kweli. Mwenyezi Mungu Alimchagua kuwa Imamu wa zama hizi. Hivyo aliielezea dunia mafundisho sahihi ya Islam. Kwa kupata lengo hili aliandika vitabu zaidi ya 80 katika lugha ya Kiurdu na Kiarabu. Kwa njia ya kutoa hotuba na kufanya mijadala na viongozi wa dini zingine alifanya kazi ya maana sana ya kueneza na kutetea Kitabu cha Mungu. Alithibitisha kwamba Islam pekee ndiyo dini illiyo sahihi na hai siku hizi inayoweza kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya mtu na Mwumba wake. Alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu Amemchagua kuwa Imam

Mahdi na Masihi Mau‘udi, sawa na bishara za Biblia, Kurani na Hadithi za Mtume[saw]. Sawa na amri ya Mwenyezi Mungu alianzisha Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, tarehe 23 Machi 1889 huko Ludhiana, India. Sasa Jumuiya yake inapatikana katika nchi 197 za dunia. Baada ya yeye kufariki, Mwenyezi Mungu Alianzisha mpango wa Ukhalifa katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa kuendeleza shughuli zake. Siku hizi Khalifa na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ndiye Hadhrat Mirza Masroor Ahmadatba.

**KUHUSU KITABU**

Kulikuwa na mtu mmoja asiyeelewa hakika ya Uimamu. Kwa kueleza kinaganaga masiala ya Uimamu wa kweli na hakika ya baiati, Seyyidna Ahmad[as] aliandika kitabu hiki kiitwacho Dharuratul Imam (Haja ya Imamu) katika Septemba 1897.

Humo alieleza kwamba Imamu wa zama ni nani na alama zake ni zipi. Vile vile alitaja katika kitabu hiki ubora wa Imamu juu ya wengine wenye kupokea ufunuo na kashfi.

Mwishowe aliandika maelezo ya kesi ya kutozwa kodi.

**SHUKRANI**


Kitabu hiki kilifasiriwa na Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya. Halafu Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania na Kenya na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbasihiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania, wakaichunguza na kusahihisha tafsiri hii na kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu sana.

Aidha ndugu kadha wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Sheikh Ansar Hussain, Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu Awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin. Tafsiri hii ni tunda la Deski ya Kiswahili.

Chaudhry Muhammad Ali M.A.
Wakilut Tasnif
Tahrik e Jadid
Rabwah. Pakistan
20.02.2013

**[Picha ya jalada la chapa ya kwanza]**



قل کفی باللہ شہیدا بینی وبینکم ومن

عندہ علم الکتاب

الحمد للہ

کہ یہ رسالہ جس کا نام ہے

# ضرورۃ الامام

صرف ڈیڑھ دن میں طیار ہو کر

مطبع

ضیاء الاسلام قادیان میں

قیمت ۲ / محصول علاوہ جلد ۷۰۰

**Jalada la chapa ya kwanza**

**Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kuwa karibu naye, na jitahidini katika njia Yake ili mpate kufaulu.**

**Na wanasema waliokufuru: Wewe si Mtume.**

**Sema: Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Shahidi baina yangu na baina yenu, na (pia) yule mwenye elimu ya Kitabu.**

**Alhamdu-lillahi**

**kijitabu hiki kiitwacho**

# Haja ya Imamu

**kikiandikwa katika siku moja na nusu tu**

**kikachapishwa katika kiwanda cha uchapaji**

**Dhiaul Islam Qadian**

**Bei: Anna 2 + gharama ya posta Nakala 700**

**chini ya usimamizi wa Bwana Hakim Fazluddin wa Bhera, mmiliki na msimamizi wa kiwanda cha uchapaji.**

# HAJA YA IMAMU

بِسْــمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[1]

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ وَ سَلَامٌ عَلٰى عِبَادِهِ الَّذِيْنَ اصْطَفٰى[2]

Baada ya haya, iwe wazi kuwa kwa mujibu wa Hadithi sahihi mtu asiyemtambua Imamu wa zama zake, kifo chake huwa ni kifo cha kijahili. Hadithi hii inaweza kumtosheleza mcha Mungu kufanya moyo wake uwe na shauku ya kumtafuta Imamu wa zama, kwani kifo cha kijahili ni mkosi unaojikusanyia maovu yote na bahati mbaya zote. Basi, kutokana na wasia huu wa Mtume[saw] hakuna budi kila anayetafuta ukweli aendelee kumtafuta Imamu wa kweli.[3]

---

[1] Kwa jina la Mweyenzi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[2] Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu, na salam ziwafikie watumishi wake aliowachagua.

[3] حدثنا عبدالله حدثنا ابى حدثنا اسود بن عامر اناابوبكر عن عاصم عن ابى صالح عن معاوية قال قال رسول الله صلى الله عليه وسلم من مات بغير امام مات ميتة جاهلية صفحه نمبر ٩٦ جلدنمبر ٤ مسند احمد و اخرجه احمد والترمذى و ابن خزيمة و ابن حبان و صححه من حديث الحارث الاشعرى بلفظ من مات وليس عليه امام جماعة فان موتته موتة جاهلية. ورواه الحاكم من حديث بن عمرو من حديث معاوية و رواه البزّار من حديث ابن عباس.

Siyo sahihi kuwa kila mtu anayepata njozi ya kweli au afunguliwaye mlango wa kupata ufunuo anaweza kuitwa jina hili. Bali hakika ya Imamu ni jambo jingine kamili na hali kamilifu timilifu isababishayo yeye kuitwa Imamu huko mbinguni. Na hii ni dhahiri kuwa mtu hawezi kuitwa Imamu kwa sababu tu ya ucha-Mungu na utakaso. Mwenyezi Mungu Anasema:

وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِيْنَ إِمَامًا ﴿٧٥﴾[4]

Basi, kama kila mcha-mungu ni Imamu, hapo waumini wote wamekuwa Maimamu; na hilo ni kinyume cha muradi wa aya. Kadhalika sawa na maneno ya Kurani Tukufu kila mpokeaji ufunuo na mwotaji wa ndoto za kweli hawezi kuwa Imamu, kwani kwa waumini wa kawaida kuna bishara hii kuwa:

لَهُمُ الْبُشْرٰى فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا[5]

yaani katika maisha ya hapa duniani, waaminio watapata neema hii kuwa mara nyingi watapata njozi za kweli au funuo za kweli. Tena katika

[4] Na utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mungu). Al-Furqaan, 25:75

[5] Wao wanazo habari njema katika maisha ya dunia. Yuunus, 10:65

sehemu nyingine ya Kurani Tukufu imo:

إِنَّ الَّذِيْنَ قَالُوْا رَبُّنَا اللّٰهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوْا

تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةُ اَلَّا تَخَافُوْا وَلَا تَحْزَنُوْا[6]

yaani wale watu wanaomwamini Mungu na kisha wanakaa imara, malaika huendelea kuwafunulia funuo za habari njema na huwatuliza, kama vile mama yake Hadhrat Musa[as] alivyotulizwa kwa njia ya ufunuo. Lakini Kurani Tukufu yaonyesha kuwa funuo na njozi za aina hiyo ni neema moja ya kiroho kwa waaminio wa kawaida, wawe wanaume au wanawake. Na kupokea funuo hizo hakuwafanyi wasimhitaji Imamu wa zama. Na mara nyingi funuo hizo zinawahusu wao wenyewe, na kwa njia ya hizo elimu hazitapakai wala hazifai kusisitizwa mno, wala haziwezi kutegemewa sana, bali pengine husababisha kujikwaa, na hamna amani kabisa katika hatari mpaka msaada wa Imam uelimishe. Ushahidi wa jambo hili umo katika siku za mwanzoni mwa Islamu, kwani mtu mmoja aliyekuwa mwandishi wa Kurani Tukufu, yeye kwa sababu ya kuwa

---

[6] Hakika wale wanaosema Mola wetu ni Mwenyezi Mungu, kisha wakaendelea kwa kudumu — huwateremkia malaika (wakiwaambia) msiogope wala msihuzunike. (Haa Miim, 41:31)

karibu na nuru ya Mtume[saw] baadhi ya wakati alikuwa akipokea funuo za Kurani Tukufu pale Imamu, yaani Nabiias, alipotaka kuiandikisha aya hiyo. Siku moja akajiliwa na wazo kuwa kuna tofauti gani kati yangu na Mtumesaw! Mimi nami napata funuo. Kwa wazo hilo akahilikishwa — imeandikwa kwamba, hata kaburi pia likamtupa nje — kama vile alivyoangamizwa Bal‘am. Hadhrat Umarra pia alikuwa akipokea funuo, lakini hakujiona chochote. Hakutaka kuwa mshirika wa Uimamu wa kweli Alioweka Mungu wa mbinguni katika ardhi; bali akajihesabu mtumishi mdogo sana na mtumwa, basi fadhili za Allah zikamfanya awe naibu wa Uimamu wa kweli. Uwais Qarni naye alikuwa akipata funuo, yeye alijifanya maskini hata kwamba akaona ni kukosa adabu kuja mbele ya jua la unabii na Uimamu. Mara nyingi Seyidna Mtume Mteule Muhammad[saw] akielekeza uso wake kwenye Yemen alikuwa anasema:

اَجِدُ رِيْحَ الرَّحْمٰنِ مِنْ قِبَلِ الْيَمَن

yaani mimi nasikia harufu nzuri ya Rahmani kutoka Yemen. Hii iliashiria kuwa nuru ya Allah imeshuka ndani ya Uwais. Lakini ni masikitiko kuwa katika zama hizi watu wengi hawatambui kuna haja ya Uimamu wa kweli, na kwa kupata

njozi chache za kweli au maneno machache ya ufunuo hujifikiria hatuna haja ya Imamu wa zama: je, tumepungukiwa nini? Na hawajali kwamba wazo hilo ni dhambi kabisa. Kwani, Mtume wetu[saw] amehakikisha kwamba ipo haja ya Imamu wa zama katika kila karne, na akasema wazi kuwa mtu yeyote atakayemjia Mwenyezi Mungu bila kumtambua Imamu wa zama zake, yeye mtu huyo atakuja akiwa kipofu na atakufa kifo cha kijahili. Katika Hadithi hii Mtume[saw] hakumtenga mpokeaji yeyote wa ufunuo au mwotaji ndoto — jambo ambalo linaeleza kwa uwazi kuwa mpokeaji ufunuo au mwotaji njozi yeyote asipojiunga na silsila ya Imamu wa zama, mwisho wake ni hatari, kwani ni dhihiri ya kwamba Hadithi hii inawahusu waaminio na Waislamu wote na kati yao waotaji ndoto na wapokeaji ufunuo wameendelea kupatikana katika kila zama. Bali ukweli ni huu kuwa katika umati wa Muhammad[saw] pengine wapo mamilioni ya watu wanaopokea funuo. Isitoshe, inathibitika kutokana na Hadithi na Kurani kuwa katika zama za Imamu wa zama kama mtu akipata funuo au njozi za kweli, hizo kwa kweli huwa ni athari ya nuru ya Imamu wa zama inayoathiri katika nyoyo zilizo tayari kuipokea. Ukweli ni huu kuwa Imamu wa

zama anapokuja duniani, maelfu ya nuru huja pamoja naye, na huko mbinguni huwepo hali ya furaha na shangwe, na kwa hali ya kiroho na mwanga kutawanyika pande zote vipawa vyema huzinduka. Basi, mtu mwenye kipawa cha kupokea funuo huanza kupokea funuo; na yule ambaye ana kipawa cha kuzingatia mambo ya dini kwa kufikiria na kutafakari huongezewa nguvu ya kufikiri; na mwenye kupenda ibada hujaliwa ladha ya kusali na kufanya ibada; na yule mtu anayejadiliana na wafuasi wa dini nyingine, yeye hujaliwa uwezo wa kutoa dalili na kutimiliza hoja. Na hayo yote kwa kweli huwa matokeo ya kutawanyika ile hali ya kiroho inayoteremka kutoka mbinguni pamoja na Imamu wa zama na kumshukia kila mwenye moyo ulio tayari kupokea. Na hii ndiyo kanuni ya kawaida na suna ya Mungu tuliyoizingatia kutoka kwa mwongozo wa Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume[saw] na tumeshuhudia kwa tajiriba zetu. Lakini zama za Masihi Mau‘udi zina sifa moja kubwa zaidi kuliko hii, nayo ndiyo kuwa katika vitabu vya manabii wa zamani na Hadithi za Mtume[saw] imeandikwa kuwa wakati wa kudhihiri Masihi Mau‘udi, kutapakaa huku nuru kutafikia kiwango kikubwa hata kwamba wanawake pia wataanza kupata

funuo na watoto wasiobalehe wataonyesha dalili za unabii[7] na watu wa kawaida wataongea kwa roho takatifu. Na hayo yote yatakuwa ni athari ya kiroho ya Masihi Mau‘udias, kama vile mwanga wa jua unapoangukia ukuta, basi ukuta hung’aa, na kama ukuta umepakwa chokaa ndipo hung’aa zaidi, na kama umebandikiwa vioo, mwanga wake huwa mkali kiasi cha kufanya macho yasiweze kuhimili. Lakini ukuta hauwezi kudai kuwa mwanga huo wote ni wake tu, kwani jua linapozama mwanga huwa unatoweka kabisa. Hivyo, nuru zote za ufunuo ni kwa sababu ya nuru za Imamu wa zama kuakisiwa, na kama si bahati mbaya wala hamna majaribio kutoka kwa Mungu, mtu mwema huweza kuelewa haraka jambo hili jepesi. Na kama, Mungu Apishe mbali, asipoelewa siri hii ya Kiungu, na baada ya kusikia taarifa za kudhihiri Imamu wa zama asipoungana naye, basi kwanza mtu huyo hamjali Imamu wa zama, kisha kutojali huko kutazalisha ugeni, na ugeni unazalisha dhana mbaya, na dhana mbaya inazalisha uadui, na kutokana na uadui, Mungu Apishe mbali, mtu anafikia hatua ya kupoteza imani. Ilivyokuwa ni kwamba wakati Mtume[saw]

---

[7] Yaani wataona njozi ya kweli. — Mwenezi

alipodhihiri walikuwepo maelfu ya maruhubani wapokeao funuo na kuona kashfi, waliokuwa wakielezea bishara za kudhihiri karibuni Nabii wa zama za mwisho, lakini wasipomkubali Imam wa zama aliyekuwa mbora wa manabii, basi radi ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ikawahilikisha na mahusiano yao yote na Mwenyezi Mungu yakakatika kabisa. Hakuna haja ya kueleza yaliyoandikwa ndani ya Kurani Tukufu juu yao. Hao ndio walioelezewa ndani ya Kurani kuwa:

وَكَانُوا مِنْ قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ[8]

Maana ya aya hii ndiyo kuwa hao watu walikuwa wakimwomba Mwenyezi Mungu msaada ili kusaidia dini; walikuwa wanapata funuo na kashfi. Ingawa hao Mayahudi waliomwasi Hadhrat Isa[as] wakadhalilika machoni mwa Mwenyezi Mungu lakini dini ya Kikristo ilipokufa kwa sababu ya kuabudu kiumbe, na ukweli na nuru vikakosekana ndani yake, basi Mayahudi wa zama hizo wakawa hawana dhambi hii kuwa kwa nini hawatanasari. Hapo mara nyingine nuru ilizalika ndani yao, wengi miongoni mwao wakaanza kupatikana wenye kupokea funuo na kashf, na miongoni mwa maruhubani wao walikuwemo watu wenye hali

---

[8]Al-Bakarah, 2:90

nzuri nao daima walikuwa wanafunuliwa kuwa nabii wa zama za mwisho na Imamu wa zama karibuni atazaliwa. Na ndiyo maana baadhi ya wanazuoni wa kiroho baada ya kufunuliwa na Mwenyezi Mungu wakaja Uarabuni. Na hata watoto walijua kuwa hivi karibuni silsila mpya itaanzishwa kutoka mbinguni. Na hiyo ndiyo maana ya aya hii:

يَعْرِفُونَهُۥ كَمَا يَعْرِفُونَ أَبْنَآءَهُمْ [9]

yaani, wanamtambua nabii yule kwa uwazi kama wanavyowatambua watoto wao. Lakini nabii huyo mwahidiwa, amani ya Mungu iwe juu yake, alipodhihiri ndipo majivumo na chuki ikawaangamiza maruhubani wengi na mioyo yao ikawa myeusi. Lakini baadhi yao walio wema wakasilimu, na Uislamu wao ukawa mzuri. Basi, hapa ni pa kuogopa, tena pa kuogopa sana. Mungu Asimfanye mwaminio yeyote kuwa mwenye mwisho mbaya kama yule Bal‘am. Ewe Mola, Uuepushe umati huu na fitina, na Uyaweke mbali macho ya Mayahudi nao. Amin tena Amin.

Hapa panafaa kukumbuka pia kuwa kama vile Mwenyezi Mungu Alivyoumba makabila na

---

[9] Al-Bakarah, 2:147

mataifa ili nidhamu ya utamaduni wa kimwili iwepo, na kwa kuoana na kuhusiana wao kwa wao wawe wanasaidiana na kuhurumiana, ndivyo hivyo alivyoweka silsila ya Unabii na Uimamu ili mahusiano ya kiroho yazalike baina ya Umati wa Muhammad[saw] na baadhi yao wawe waombezi wa baadhi wengine.

Sasa, swali moja la muhimu ni hili kuwa Imamu wa zama yu nani na alama zake ni zipi? Na yeye ana kipaumbele gani juu ya wanaopata ufunuo, ndoto na kashf? Jibu lake ni kuwa Imamu wa zama ni yule mtu ambaye Mwenyezi Mungu Akiwa mdhamini wa ulezi wake wa kiroho Anatilia asili yake mwanga wa Uimamu, basi yeye huwashinda wataalamu wa mantiki na falasfa wa dunia nzima kwa kujadiliana nao kwa kila namna. Yeye akipata uwezo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hujibu makinzani magumu sana ya kila namna kwa njia nzuri kabisa hata kwamba hatimaye hakuna budi kukubali kuwa asili yake imekuja duniani ikiwa na nyenzo zote za kuirekebisha dunia hii. Kwa hiyo, yeye haaibiki mbele ya adui yeyote. Yeye huwa kiroho Amiri jeshi wa jeshi la Muhammad. Mwenyezi Mungu Hutaka kuushindisha dini mara nyingine kwa mkono wake. Na watu wote wanaokuja chini ya

bendera yake nao hujaliwa nguvu za hali ya juu sana. Na anajaliwa masharti yote ya lazima kwa ajili ya marekebisho, na elimu zote za lazima kwa kuondolea mbali makinzani na kubainisha sifa bora za Islamu. Hata hivyo, kwa vile Mwenyezi Mungu Anajua kuwa yeye itabidi apambane pia na watu wa dunia wasio na adabu na wenye midomo michafu, hivyo yeye hupewa nguvu ya hulka njema ya daraja la juu, na moyoni mwake huwa huruma ya kweli kwa binadamu. Na nguvu ya hulka siyo muradi wake kuwa anatumia upole kila mahali bila sababu yoyote. Kwani hiyo ni kinyume cha kanuni ya hekima ya hulka njema. Bali muradi wake ni kwamba wenye hulka njema hali yao haiwi kama hali ya watu wenye mioyo midogo wanaogeuka haraka kitabia kwa kuhamaki kwa sababu ya maneno yasiyo na adabu ya adui, na nyusoni mwao hudhihirika athari mbovu sana za adhabu iumizayo ambayo yaitwa ghadhabu, na midomoni mwao huendelea kutoka bila kujiweza na pasipofaa maneno ya hasira na uchochezi. Naam, kulingana na hali na mahali wanatumia pia maneno makali kama tiba; lakini wakati wa matumizi hayo, moyo wao hauungui wala haiwi hali ya hamaki wala halitoki povu midomoni. Naam wakati mwingine ili kuonyesha heba

hujifanya wamekasirika, ilhali moyo unakuwa katika hali ya kutulia na kuchangamka na kufurahika. Ndiyo maana, ingawa Hadhrat Isa[as] mara nyingi ametumia maneno makali kwa alioongea nao  kama vile kuwaita nguruwe, mbwa, wasio na imani, waovu na kadhalika, lakini hatuwezi kusema kuwa, Mungu Apishe mbali, yeye hakuwa na hulka njema, kwani yeye ndiye aliyekuwa anafunza hulka njema na kusisitiza kutumia upole. Bali, maneno hayo yaliyokuwa yakitoka midomoni mwake hayakuwa kwa sababu ya ghadhabu, hamaki na hasira ya kimajnuni, bali yalitumika barabara palipofaa kwa kumakinika na kutulia. Ilmuradi, kuwa mkamilifu katika hulka njema ni lazima kwa Maimamu. Na endapo neno kali litamkwe pasipokuwa na tabia kali na hasira ya kimajnuni pale pafaapo sawa na haja, kufanya hivyo haitakuwa kinyume cha hali ya hulka njema. Na yafaa ielezwe kuwa wale ambao Mkono wa Mwenyezi Mungu Unawafanya Maimamu, katika tabia yao ya asili nguvu ya Uimamu huwa inawekwa. Na kama vile sawa na aya hii:

أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ[10]

[10] Aliyekipa kila kitu umbo lake. Twaa Haa, 20:51

Mwenyezi Mungu Alivyokwisha mjalia mapema kila mnyama na ndege ile nguvu aliyoijua Mwenyenzi Mungu kuwa atalazimika kuitumia, vivyo hivyo, ndani ya watu ambao Mwenyezi Mungu Ana elimu kuwa watapewa kazi za Uimamu, vinavyowekwa mapema vipawa mbalimbali vya kiroho; na nguvu zitakazohitajika hapo baadaye, mbegu ya nguvu hizo hupandwa ndani ya maumbile yao. Naona nguvu zifuatazo ni lazima ziwepo ndani ya Maimamu kwa ajili ya faida ya wanadamu:

Ya kwanza, nguvu ya hulka njema: Kwa kuwa Maimamu hukabiliana na wahuni wa aina mbalimbali na watu duni na wenye midomo michafu, hivyo ni lazima wawe na nguvu ya hulka njema ili wasipatwe na hasira ya kinafsi wala hamaki ya kimajnuni na ili watu wasikose baraka zao. Ni jambo la aibu sana kuwa mtu akiitwa rafiki wa Mungu, ashikwe na hulka mbovu, na asiweze kabisa kuvumilia maneno makali. Na yule anayejiita Imamu wa zama akiwa ni mtu mwenye mwenendo hafifu hata kwamba kwa sababu ya mambo madogo madogo hutokwa na povu, macho yanaonyesha hasira, yeye mtu huyo hawezi katu kuwa Imau wa zama. Hivyo, yalazimu yaliyoelezwa katika aya hii yalingane naye

kikamilifu:

إِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ۝[11]

Ya pili ni nguvu ya Uimamu inayomfanya aitwe Imamu, yaani shauku ya kusonga mbele katika mambo mema na matendo mema, maarifa ya Mungu na mapenzi ya Mungu. Yaani, roho yake isipende upungufu wowote, wala isiridhike na hali yoyote pungufu, na asikie uchungu na udhia akizuiwa asipate maendeleo. Hii ni nguvu ya kiasili inayokuwemo ndani ya Imamu. Na hata kama kwa bahati watu wasifuate elimu na ujuzi wake, wala wasifuatie nuru yake hata hivyo yu bado Imam tu kwa nguvu yake ya asili. Ilmuradi, maarifa haya ya ndani yanastahili kuzingatiwa kuwa Uimamu ni nguvu iliyowekwa ndani ya asili ya yule mtu anayekusudiwa na Mwenyezi Mungu kwa kazi hiyo. Na kama tukifasiri neno 'Uimamu' twaweza kusema ni "nguvu ya kutangulia". Ilmuradi, hiki si cheo cha muda kinachopatikana baadaye, bali kama vile nguvu ya kuona, nguvu ya kusikia na nguvu ya kuelewa zilivyo, ndivyo hivyo ilivyo hii nguvu ya kuendelea mbele na kuwa katika daraja la kwanza katika mambo ya

[11] Na bila shaka una tabia njema, tukufu. Al-Qalam, 68:5

Mungu, na kwenye maana hiyo neno la Uimamu linaashiria.

Nguvu ya tatu ni wasaa katika elimu ambao ni muhimu sana kwa Uimamu na ni sifa maalumu ya lazima. Kwa kuwa maana ya Uimamu inataka kusonga mbele katika kuzingatia kweli zote na maarifa yote na mambo yaliyo ya lazima ya upendo na unyofu na uaminifu, na kwa shabaha hiyo anatumikisha nguvu zake nyingine zote na daima Imamu hushughulikia kuomba dua hii:

رَبِّ زِدْنِيْ عِلْمًا [12]

na mapema hisia zake zina uwezo kwa mambo hayo ndiyo maana kwa fadhili za Mwenyezi Mungu yeye hujaliwa wasaa katika elimu takatifu za dini, na katika zama zake hakuna mwingine yeyote aliye sawa naye katika kujua maarifa ya Kurani na sifa za kunufaisha na kukamilisha hoja. Na rai yake iliyo sahihi inasahihisha elimu za wengine. Na kama katika kueleza kweli za dini, rai ya mtu yeyote ikipingana na rai yake, hapo ukweli huwa upande wake, kwani kuzitambua elimu za kweli, nuru ya busara humsaidia, na nuru hiyo yenye miale imetametayo hajaliwi wengine.

---

[12] Mola wangu, nizidishie elimu. Twaa Haa, 20:115

ذٰلِكَ فَضۡلُ اللّٰهِ يُؤۡتِيۡهِ مَنۡ يَّشَآءُ ؕ[13]

Hivyo, kama vile kuku anavyoatamia mayai na kutotoa vifaranga na kwa kuvikumbatia chini ya mbawa zake na huvitilia sifa zake, ndivyo hivyo mtu huyu kutokana na elimu zake za kiroho anavyoendelea kuwapatia wakaao naye elimu na kuwaongezea yakini na maarifa. Lakini siyo lazima kwa wapokeao funuo na watawa wengine wawe na wasaa wa elimu hivyo, kwani hao huwa hawakabidhiwi malezi ya kielimu ya wanadamu. Na haidhuru kama hao watawa na waotao ndoto wamebakiwa na upungufu wa elimu na ujahili kidogo. Kwani wao sio manahodha wa safina yoyote bali wenyewe wanamhitaji nahodha. Naam, hawapaswi kujiingiza katika upuuzi kuwa eti hatumhitaji nahodha huyu wa kiroho, sisi wenyewe tuko hivi na hivi. Yapasa wazingatie kwamba haja wanayo tu jinsi mwanamke anavyomhitaji mwanamume. Mungu Amemwumba kila mmoja kwa kazi maalum. Hivyo basi, yule ambaye hakuumbwa kwamba awe Imam, akidai hivyo atawfanya watu wamcheke. Kama walii mmoja jahili

---

13 Hiyo ni fadhili ya Mwenyezi Mungu, Humpa Amtakaye. Al-Jumu‘a, 62:5

alivyochekwa mbele ya mfalme. Kisa chenyewe ni kuwa katika mji fulani kulikuwa na mtawa mmoja aliyekuwa mwema na mcha-Mungu, lakini alikuwa hana elimu. Mfalme alimwamini sana, lakini kwa sababu yeye hakuwa na elimu, waziri hakumwamini. Safari moja, mfalme na waziri walikwenda kuonana naye. Yeye bwana huyo akipiga domo akaongelea jambo fulani la historia ya Islamu na akamwambia mfalme kuwa katika umati huu Iskander wa Rumi pia amepita naye aliyekuwa mfalme mkubwa. Hapo waziri akapata nafasi ya kumtolea kosa walii huyo, akasema haraka, mheshimiwa mfalme, angalia, daruweshi huyu zaidi ya sifa za uwalii ana ujuzi wa historia pia! Hivyo basi, Imamu wa zama hahitaji sana funuo kukabiliana na wapinzani na waulizaji maswali kadri anavyohitaji nguvu ya kielimu. Maana, wako wengi wanaoleta upingamizi wa kila aina dhidi ya sheria kulingana na utabibu, sayansi, fizikia, jiografia, vitabu vya Kiislamu, akili na maandiko. Na Imamu wa zama huitwa mhifazi wa Jumuiya ya Waislamu na anafanywa na Mwenyezi Mungu mlinzi wa bustani hii, na anawajibikiwa kuondolea mbali kila upinzani na kufumba midomo ya kila mpinzani; na si hiyo tu, bali ni faradhi yake kuwa asijibu tu hoja za

upinzani bali pia audhihirishie ulimwengu uzuri na ubora wa Uislamu.

Hivyo basi, mtu kama huyo anastahili kuheshimiwa, na yu kama jiwe lile la mwanafalsfa linaloaminiwa kukigeuza kinacholigusa kuwa dhahabu, kwani kwa dhati yake uhai wa Uislamu unadhihirika. Yu fahari ya Islam na hoja ya Mwenyezi Mungu kwa watu wote. Na haijuzu kwa yeyote kutengana naye, kwani yeye kwa utashi na idhini ya Mwenyezi Mungu huwa mlinzi wa heshima ya Uislam, mwenye kuwahurumia Waislamu wote, na hujikusanyia sifa zote kamilifu za dini. Yuafaa katika kila uwanja wa kuangushana mwereka baina ya Islam na ukafiri. Pumzi zake tukufu huua ukafiri. Yu kitu kizima, wengine wote ndio shehemu zake.

او چو کل و تو جزئی نے کلی
تو ہلاک استی اگر از وے بگسلی

Kwa kuwa Yu kitu kizima, nawe u sehemu tu; si kitu kizima basi, ukitengana naye utaangamia.

Nguvu ya nne ni azma ambayo ni ya lazima sana kwa Imamu wa zama. Azma, muradi wake ni kutochoka katika hali yoyote ile, kutokata tamaa wala kutolegea katika nia. Baadhi ya wakati Manabii, Mitume, Wahaddathina ambao

wanakuwa Maimamu wa zama hupata majaribio na kidhahiri wananaswa katika misiba kana kwamba Mwenyezi Mungu Amewaacha na Amekusudia kuwaangamiza; na wakati mwingine wahyi na funuo unakatika, na kwa muda fulani hawafunuliwi wahyi. Na baadhi ya wakati matabiri yao yanadhihiri kama majaribio. Na ukweli wao haudhihiriki kwa watu; na pengine hata muda wa kupata makusudio yao huchelewa sana. Pengine hao wanakuwa duniani kama waliotengwa na walioachwa bila msaada na waliolaaniwa na waliofukuzilia mbali. Na kila mtu anayemtukana hudhani kana kwamba anafanya kitendo cha thawabu sana. Na kila mmoja anawachukia na kuwakirihi na hataki kupokea hata maamkizi ya salam zao. Lakini katika nyakati hizo ndipo azma yao hujaribiwa; hawavunjiki moyo kwa majaribio hayo wala hawalegei katika kazi zao mpaka msaada wa Mungu unawadia.

Nguvu ya tano ni kumwendea Mungu, ambayo ni lazima kwa Imamu wa zama. Muradi wa mwelekeo kwa Mungu ni kuwa waja hao katika nyakati za misiba na majaribio na pia wanapokabiliana na adui mkali na kuombwa kuonyesha ishara, au ipo haja ya ushindi, au wakiwajibikiwa kumhurumia fulani, hapo

humwelekea Mwenyezi Mungu, na wanamwelekea hivi kwamba kwa dua zao zilizojaa unyofu, ikhlasi, upendo, uaminifu na azma thabiti, wanataharaki malaika waliomkurubia Mungu, ndipo kwa maombi ya kujinyenyekeza ya hao waja vinazalika vilio vyenye uchungu vinavyohangaisha malaika, kisha kama vile baada ya joto kali kufikia kilele chake, mawingu yanavyoanza kudhihirika mbinguni mwanzoni mwa masika, ndivyo hivyo joto la mwelekeo wao kwa Mungu, yaani joto la bidii yao kubwa ya kuelekea kwa Mwenyezi Mungu, linavyoanza kufanyiza jambo fulani huko mbinguni, na kudura zabadilika na matakwa ya Mungu yashika hali nyingine mpaka pepo baridi za kudra ya Mwenyezi Mungu huanza kuvuma. Na jinsi ambavyo kile kinachosababisha homa chazalika kwa kanuni ya Mwenyezi Mungu, kisha msahala nao huondolea sababu ya homa kwa amri ya Mwenyezi Mungu, hivyo ndivyo ilivyo athari ya waja wa Mungu kuelekea kwake.

آں دعائے شیخ نے چوں ہر دعاست

فانی است و دستِ او دستِ خداست

Dua ya sheikh yule sio kama kila dua ya kawaida; ameshajipoteza katika Mungu na mkono wake ni

mkono wa Mungu.

Na Imamu wa zama kumwendea Mungu, yaani mwelekeo wake kwa Mungu huwa ina nguvu nyingi na unaathiri haraka sana kuliko ule wa mawalii wote. Mathalan, Musa[as] alikuwa Imamu wa zama zake, na Balaamu alikuwa walii wa wakati wake aliyebahatika kufanya maongezi na Mungu na pia maombi yake yalikuwa yakikubaliwa, lakini Balaamu aliposhindana na Musa, mashindano hayo yakamwangamiza Balaamu kama vile upanga mkali unavyokatia mbali kichwa. Na kwa kuwa Balaamu mwenye bahati mbaya hakujua hekima hii kuwa hata kama Mwenyezi Mungu Akiongea na mtu na kumfanya mpendwa wake na mtawa, lakini yeye mtu huyo anaposhindana na yule aliyemzidi katika fadhili, bila shaka huyo ataangamia na hapo ufunuo wowote hautamfaa kitu wala kupokelewa maombi hakutamsaidia katu. Na huyo alikuwa ni Balaamu mmoja tu, lakini mimi najua kuwa wakati wa Mtume wetu[saw] maelfu ya Balaamu walihilikishwa, kama maruhubani wengi wa Mayahudi walivyokuwa baada ya kufa dini ya Kikristo.

Ya sita ni mfululizo wa kashfi na funuo ambao huwa ni lazima sana kwa ajili ya Imamu wa zama.

Imamu wa zama mara nyingi hupokea elemu, mambo ya kweli na maarifa kwa njia ya funuo. Na funuo zake haziwezi kulinganishwa na zile za wengine, maana, katika hali na idadi huwa za kiwango cha juu sana asichoweza mtu kukizidi. Kwazo elimu zinafunuka na maarifa za Kurani zafahamika, mambo magumu ya dini na matatizo hutatuliwa na hudhihirika bishara za daraja ya juu zinazoweza kuwaathiri wapinzani wa dini zingine. Ilmuradi, walio Maimamu wa zama kashfi na funuo zao haziishii mpaka kwa mambo ya watu binafsi bali huwa zenye manufaa makubwa na baraka nyingi kwa kusaidia dini na kuimarisha imani. Mwenyezi Mungu huongea nao kwa wazi kabisa na hujibu dua yao. Na pengine maongezi ya maswali na majibu hupatikana, na katika kipindi kimoja huanza mfululizo wa kutolewa jawabu baada ya ulizo, tena jawabu baada ya ulizo, tena jawabu baada ya ulizo, kwa ufunuo safi, mtamu na fasaha, hata kwamba afunuliwaye hufikiri kana kwamba anamwona Mwenyezi Mungu. Na ufunuo wa Imamu wa zama hauwi kama mrushaji mawe arushe jiwe kwa siri na kukimbia, na isijulikane alikuwa nani na amekwenda wapi; bali Mwenyezi Mungu Humkurubia sana, na kiasi fulani hufunua pazia

kwenye uso wake mtakatifu na wenye kung’aa. Na hali hii hawajaliwi wengine, bali hao baadhi ya wakati wanajikuta kana kwamba wanadhihakiwa na mtu. Na matabiri anayofunuliwa Imamu wa zama yanazishinda ghaibu, yaani, yanazitamalaki ghaibu kwa kila jiha jinsi mpanda farasi hodari anavyoomtamalaki farasi. Na nguvu hii na mdhihirisho huu hujaliwa kwa ufunuo wao ili funuo zao takatifu zisiwe na mashaka ya kuchanganyikiwa na funuo za kishetani na ili ziweze kuwa hoja kwa wengine.

Iwe wazi kuwa kufunuliwa funuo za kishetani ni jamo la kweli; wanazipata hizo baadhi ya wale wasiokomaa kiutawa. Na kuna kujizungumza pia kunakoitwa ndoto zilizovurugika, na yule anayekana habari hii anaipinga Kurani Tukufu. Kwani sawa na Kurani Tukufu funuo za kishetani zipo. Na Mwenyezi Mungu Anasema kuwa maadamu mtu hatakasiki nafsi yake kikamilifu, anaweza kupata ufunuo wa kishetani na aweza kuwa chini ya aya:

عَلٰى كُلِّ اَفَّاكٍ اَثِيْمٍ ﴿۲۲۳﴾[14]

[14] (Mashetani wanateremka) juu ya kila mzushi mkubwa, mwenye dhambi. Ash-Shu‘araa, 26: 223

Lakini watu wema huarifiwa papo hapo juu ya wasiwasi wa kishetani.

Ni bahati mbaya kuwa baadhi ya mapadri wamejasiri kuandika katika vitabu vyao wakieleza tukio la shetani kumpeleka Hadhrat Isa[as] huko mlimani kwamba hili halikuwa jambo la dhahiri ambalo dunia ingeliona na Mayahudi nao wangelishuhudia, bali Yesu alipata ufunuo wa kishetani mara tatu ambao yeye hakuukubali. Lakini mwili wetu unatetemeka kusikia maelezo ya aina hii ya Injili. Lo! Masihi na ufunuo wa kishetani!! Naam, kama tusiyakubali maongezi hayo ya kishetani kuwa ufunuo wa kishetani na tudhani kuwa shetani akijipatia mwili akakutana na Yesu, hapa swali linazuka kuwa kama shetani ambaye ni nyoka wa siku nyingi kweli alijidhihirisha katika sura ya kimwili na kwa umbo la kidhahiri akawa mtu na akasimama karibu na hekalu takatifu la Mayahudi ambalo pembezoni mwake mamia ya watu waliishi, bila shaka maelfu ya watu wangelikusanyika kumuona; bali ingelifaa Yesu angewaita Mayahudi waje akawaonyeshe shetani ambaye makundi mengi yalimkataa kuwepo kwake. Na kuonyesha shetani kungekuwa ni mwujiza wa Yesu ambao ungesababisha watu wengi

kuongoka, na wakuu waheshimiwa wa ufalme wa Kirumi bila shaka wangemkubali Yesu ambao ungesababisha watu wengi kuongoka, na wakuu waheshimiwa wa ufalme wa Kirumi bila shaka wangemkubali Yesu baada ya kumuona shetani na kisha kwa kumshuhudia akiruka. Lakini haikuwa hivyo. Hii inahakikisha kuwa hayo yalikuwa ni maongezi ya kiroho ambayo kwa maneno mengine tunaweza kusema ni ufunuo wa kishetani. Lakini wazo lanijia pia kuwa ndani ya vitabu vya Mayahudi watu wengi wakorofi nao wameitwa shetani. Kwa kutumia methali hii Yesu pia akamwita mwanafunzi wake mtukufu kuwa shetani ambaye mistari michache tu kabla ya kuelezea tukio hili katika Injili akapewa funguo za Peponi.

Hivyo, inawezekana kuwa huenda Myahudi mmoja mwenye khulka za kishetani akamfikia Yesu na yeye kama alivyomwita Petro jina shetani, akamwita yeye pia shetani. Na Mayahudi walikuwa wakifanya pia ukorofi wa aina hii, na kuuliza maswali kama hayo ndiyo tabia ya Mayahudi. Na hii pia inawezekana kwamba kisa chote hiki kiwe uongo mtupu kilichoandikwa kwa makusudi au kwa kudanganyika, kwani Injili hizi si Injili za Yesu wala hazikusadikishwa naye, bali

ziliandikwa tu na wanafunzi wake au mtu mwingine sawa na mawazo na akili yake tu, na ndiyo maana zinahitilafiana pia. Hiyo twaweza kusema kuwa katika kuandika mawazo kama hayo waandishi wakapata kukosea jinsi walivyokosea baadhi ya waandishi wa Injili walipodhania kuwa Yesu akafia msalabani.[15] Makosa kama hayo yalikuwamo katika tabia ya wanafunzi, maana Injili inatuarifu kuwa akili zao hazikuwa nyepesi. Ubovu wa hali zao unatolewa ushahidi na Yesu mwenyewe kuwa hao walikuwa dhaifu katika fahamu na utambuzi na nguvu ya kutenda. Kwa vyovyote vile, hii ni kweli kuwa ndani ya mioyo ya watu wema fikara ya kishetani haiwezi kuimarika. Na hata kama wasiwasi kidogo ukipitapita uusogolee moyo wao, papo hapo fikara hiyo ya kishetani huondolewa na kufukuziliwa mbali na doa lolote chafu haliwapati. Wasiwasi kama huo ufananao na wazo hafifu usiopevuka umeitwa Taaif katika Kurani Tukufu. Na katika lugha ya Kiarabu hilo laitwa Taaif, Tauf, Tayyif

---

[15] Miongoni mwa Injili nyingi za Wakristo kuna Injili moja waliyo nayo mpaka leo ilimoandikwa kuwa Yesu hakufa msalabani. Usemi huu ni sahihi, kwani marhamu ya Isa inaisadikisha ambayo imetajwa na mamia ya matabibu. — Mwandishi.

na Taif pia. Uhusiano wa wasiwasi huo na moyo huwa ni hafifu sana kana kwamba hakuna kabisa. Au tuseme hivi kuwa jinsi kivuli cha mtu kutoka mbali kinavyokuwa hafifu sana ndivyo ulivyo wasiwasi huu. Na yumkini shetani mlaaniwa alikusudia kuingiza wasiwasi hafifu wa aina hii ndani ya moyo wa Yesu, naye kwa nguvu ya Unabii akaundoa wasiwasi huo. Nasi tumelazimika kusema hayo, kwani kisa hiki hakimo ndani ya Ma-Injili tu, bali kimo pia ndani ya vitabu vyetu vya Hadithi zilizo sahihi ambamo mmeandikwa kuwa:

عن محمد بن عمران الصيرفى قال حدثنا الحسن بن عليل العنزى عن العباس بن عبدالواحد. عن محمد بن عمرو. عن محمد بن مناذر. عن سفيان بن عيينة عن عمرو بن دينار. عن طاؤس عن ابى هريرة قال جاء الشيطٰن الٰى عيسَى. قال الست تزعم انک صادق قال بلٰى قال فاوف على هذه الشاهقة فالق نفسک منها فقال ويلک الم يقل اللّٰه يا ابن ادم لا تبلنى بهلاکک فانى افعل ما اشاء

Yaani, imesimuliwa na Muhammad bin Imrani Sairafii, naye amesimuliwa na Hassan bin ‘Aliil Al-anzi, na Hassan kutoka kwa Abbasi bin Abdul Wahid, na Abbasi kutoka Muhammad bin Amri, na Muhammad bin Amri alisimuliwa na Muhammad bin Munadhir, naye akasimuliwa na Sufian bin Uyainah, naye alisimuliwa na Amr bin Diinar, Amri bin Diinar akasimuliwa na Taus na Taus alisimuliwa na Abu Huraira ambaye akasema shetani alimfikia Isa, akasema je wewe

hudhani kuwa u mkweli? Akasema naam, ni mkweli. Shetani akasema kuwa kama hii ni kweli, panda juu ya mlima huu, kisha ujiangushe chini kutoka juu yake. Hadhrat Isa akasema, ole wako, je, hujui kwamba Mungu Amesema usinijaribu kwa kifo chako, kwani, Mimi Hufanya Ninalopenda. Sasa ni dhahiri kuwa shetani huenda alikuja kwake kama Jibriili anavyowafikia mitume. Maana, Jibriili haji kama anavyokuja mtu akikaa ndani ya gari au juu ya farasi wa kukodi, huku amevaa kilemba na amejitanda shuka. Bali, kuja kwake ni kwa njia ya kiroho. Sasa shetani ambaye ana daraja la chini na ni dhalili sana, iweje aweze kuja waziwazi kibinadamu. Kwa uchunguzi huu yalazimu kukubali aliyoyasema Draper. Lakini tunaweza kusema kuwa kwa nguvu ya unabii na nuru ya ukweli Hadhrat Isa[as] kamwe hakuuachia ufunuo wa kishetani nafasi ya kumkaribia, na mara akashughulikia kuuondoa na kuutupilia mbali. Na kama ambavyo giza haliwezi kuikabili nuru, ndivyo ambavyo shetani hakuweza kuthubutu mbele yake na akakimbia, na hii ndiyo maana sahihi ya aya:

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ [16]

Maana, usultani wa shetani, yaani mamlaka yake, huwa juu ya wale wanaokubali wasiwasi na ufunuo wa kishetani. Lakini wale ambao wanamjeruhi shetani kwa mshale wa nuru kutoka mbali na kumkemea na kumkaripia vikali, wala hawayafuati maneno yake ya kuropoka, hao hawatawaliwi na shetani. Lakini kwa vile Mwenyezi Mungu Anataka kuwaonyesha ufalme ya mbingu na ardhi, na shetani yumo katika ufalme wa ardhi, hivyo basi ili kukamilisha duara la kushuhudia viumbe, yalazimu hao wapate kumwona kiumbe huyu wa ajabu sura yake anayeitwa shetani na kusikia maneno yake. Kwa sababu utakaso wao na takato lao halipati doa chafu asilani. Shetani kwa mbinu yake ya zamani ya kutia wasiwasi alimuomba kwa ukorofi Hadhrat Masihi[as] jambo moja lakini tabia yake takatifu ikalikatalia ombi hilo mara moja wala haikulikubali. Hiyo haikumvunjia heshima. Je, wahuni hawapati wakati mwingine kuzungumza mbele ya wafalme? Hivyo ndivyo kwa kiroho shetani alivyotia maneno yake ndani ya moyo wa

[16] Hakika watumishi wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao. Al-Hijr, 15:43

Yesu. Yesu hakuukubali ufunuo huo wa kishetani, bali akaukatilia mbali. Basi hili ni jambo la kusifiwa; kulikosoa ni ujinga na ni kutojua hekima za kiroho. Lakini jinsi Yesu alivyofukuzilia mbali wazo la kishetani kwa kiboko cha nuru na kudhihirisha uchafu wa ufunuo wake, hii siyo kazi ya kila mtawa na sufii. Sayyid Abdul Qadir Jilanira amesema kuwa safari moja mimi pia nilipata ufunuo wa kishetani. Shetani alisema: “Ewe Abdul Qadir ibada zako zimekubaliwa, sasa kilicho haramu kwa wengine ni halali kwako, huna haja ya kusali sasa, chochote uanachotaka fanya tu. Hapo mimi nikasema: Ewe shetani, ondoka, vipi naweza kuhalalishiwa mambo ambayo haya kuhalalishwa kwa Mtumesaw. Ndipo shetani pamoja na arshi yake ya dhahabu akatoweka mbele ya macho yangu. Sasa, ikiwa mtawa na mtu wa pekee wa Mungu kama Abdul Qadir alipata ufunuo wa kishetani, watu wengine wa kawaida ambao hawajatimiliza bado safari yao ya kiroho wanawezaje kusalimika nao? Na wamekuwaje na macho yenye nuru ili kutambua ufunuo wa kishetani kama Sayyed Abdul Qadir na Hadhrat Masihias. Ikumbukwe kuwa wale makuhani waliokuwepo Uarabuni kabla ya kudhihiri Mtumesaw, hao walikuwa wakipata

funuo za kishetani kwa wingi. Na baadhi ya wakati walikuwa wakatoa matabiri pia kwa funuo. Na ajabu ni kwamba baadhi ya matabiri yao yalikuwa ya kweli pia. Vitabu vya Kiislam vimejaa visa hivyo. Kwa hiyo, mtu anayekataa kuwepo kwa ufunuo wa kishetani, yeye mtu huyo anayakataa mafundisho ya manabii wote na anakataa utaratibu wa unabii. Imeandikwa ndani ya Biblia kuwa safari moja manabii mia nne walipata ufunuo wa kishetani, na kwa ufunuo uliokuwa hila ya jini mweupe wakatoa utabiri wa ushindi wa mfalme. Hatimaye mfalme huyo katika vita hivyo akauwawa kwa fedheha kubwa na ushinde mbaya. Na Nabii mmoja aliyepokea ufunuo kutoka kwa malaika Jibriil yeye alitoa bishara hii kuwa mfalme atauawa na mbwa watakula nyama yake na ushinde mkubwa utapatikana, na habari hii ikatokea kuwa ya kweli. Lakini bishara ya Manabii wale mia nne ilitokea kuwa uwongo.

Hapa swali linazuka kuwa iwapo funuo za kishetani pia zinapatikana kwa wingi, basi ufunuo wenyewe hauaminiki, na ufunuo wowote haupasi kutegemewa. Kwani, huenda huo uwe wa kishetani, hususan ukizingatia kuwa hata Masihi, Mtume mwenye imara pia alipata kuikabili hali

kama hii. Basi, hili linawavunja kabisa moyo wapokeaji wa funuo. Je, ufunuo zinabakia kuwa balaa tu? Jibu la swali hili ni kwamba hakuna sababu ya kuvunjika moyo. Ilivyo kanuni ya kadri ya Mwenyezi Mungu iliyomo duniani ni kwamba kwa kila johari nzuri kuna vitu vya kuiga pia. Hebu, angalieni, kuna lulu zinazotoka mtoni, na ziko nyingine zilizo rahisi wanazotengeneza watu na kuziuza. Sasa, kwa vile duniani kuna lulu za kuiga pia, biashara ya lulu za kweli haiwezi kukoma, kwani wauza lulu waliojaliwa busara na Mwenyezi Mungu wanatambua mara moja kuwa hiyo ni kweli na hiyo ni ya kuiga. Basi mtambuzi wa lulu za ufunuo ndiye Imamu wa zama. Kwa kukaa naye mwanadamu mara moja huweza kutofautisha kati ya asili na ya kuiga. Enyi masufii, na enyi walionasa katika kemia, kanyageni katika njia hii mkiwa macho, na kumbukeni kuwa ufunuo wa kweli unaofunuliwa hasa na Mwenyezi Mungu huwa na alama zifuatazo:

1. Huo unafunuliwa katika hali ambapo moyo wa mtu kwa kuyeyuka na moto wa uchungu hutiririka kama maji safi ukimwelekea Mwenyezi Mungu. Huko ndiko inakoashiria Hadithi kuwa Kurani Tukufu ilishuka katika hali ya huzuni, hivyo

nyinyi nanyi isomeni kwa moyo wa huzuni.

2. Ufunuo wa kweli huleta hali ya ladha na furaha, na kwa sababu isiyoelezeka hujalia yakini, na kama msumari wa chuma huingia ndani ya moyo, na ibara yake huwa fasaha isiyo na kosa lolote.

3. Ndani ya ufunuo wa kweli mna shani na adhama, na kwa huo moyo hupata pigo imara na huteremka moyoni kwa nguvu na sauti yenye heba. Lakini ndani ya ufunuo wa uongo mna sauti hafifu kama za wezi, mahanithi na wanawake, maana shetani ni mwizi, na hanithi na mwanamke.

4. Ufunuo wa kweli una athari ya nguvu za Mwenyezi Mungu ndani yake, na ni lazima pia ziwemo ndani yake bishara ambazo zitimie pia.

5. Ufunuo wa kweli unaendelea kumfanya mtu kuwa mwema siku hadi siku na huondoa taka na uchafu wa ndani na huzikuza hali zake za kihulka.

6. Nguvu zote za ndani za Mtu zawa shahidi kwa ufunuo wa kweli na kila nguvu hupata mwanga mpya na mtukufu, na mtu huona ndani yake badiliko, na maisha yake ya kwanza yanakufa na huanza maisha mapya, naye huwa ni njia ya kuwapatia wanadamu huruma kwa jumla.

7. Ufunuo wa kweli hauishii kwenye sauti moja,

maana sauti ya Mungu huwa unafululiza. Yeye ndiye Mpole sana. Anapoelekea kwa yeyote. Huongea naye na Hutoa majibu ya maswali. Na mtu anaweza kupata majibu ya maombi yake wakati uo huo na mahali hapo hapo, ingawa maongezi hayo wakati mwingine yanakatika pia kwa muda.

8. Mwenye kupata ufunuo wa kweli kamwe hawi mwoga, na haogopi kumkabili mdai yeyote wa kupokea ufunuo, hata kama awe mpinzani mkali namna gani; anajua kuwa Mungu yu pamoja naye na Atamshinda huyo kwa kumfedhehesha sana.

9. Ufunuo wa kweli mara nyingi huwa ni njia ya kujulia elimu na maarifa, maana Mungu hapendi mja wake anayefunuliwa kumwacha bila elimu na jahili.

10. Ufunuo wa kweli huwa na baraka nyingine nyingi. Anayeongea na Mungu hujaliwa heshima kwa ghaibu na hujaliwa adhama.

Zama hizi ni zama mbovu sana hata kwamba wengi wapendao falsafa na wasiomwamini Mungu na wafuasi wa dhehebu la Barahmu wanakana ufunuo huo. Wengi wameondoka dunia hii katika hali ya kukataa huku. Lakini hakika yenyewe ni kuwa ukweli ni ukweli tu hata kama

dunia nzima iukatilie mbali; na uongo ni uongo tu hata kama dunia nzima iusadikishe. Wale watu ambao wanamwamini Mwenyezi Mungu na wanamtambua kuwa ndiye mpangaji wa walimwengu na wanamtambua kuwa ndiye mwenye kuona, mwenye kusikia na mwenye kujua, ni upumbavu wao kuwa baada ya ikirari hizo zote wakatae maongezi ya Mwenyezi Mungu. Je yule anayeona, anayejua, na bila njia za dhahiri Anaijua kila chembe, hawezi kusema? Ni kosa pia kusema kwamba nguvu yake ya kusema alikuwa nayo hapo zamani lakini sasa imeishia, kana kwamba sasa sifa yake ya kuongea haiendelei, bali imeishia zamani. Lakini kusema hivi kunakatisha tamaa kabisa. Kama sifa za Mwenyezi Mungu pia baada ya kuendelea kwa zama fulani kisha zatoweka hata alama yake yoyote haibaki, basi sifa nyingine zinazosalia nazo ziko hatarini. Nasikitikia akili hizi na itikadi hizi za wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu kisha wanachukua kisu na wakikata sehemu yake moja muhimu wanaitupilia mbali. Ni sikitiko kuwa Maariya walifunga ufunuo wa Mwenyezi Mungu mpaka kwa Veda tu, lakini hata Wakristo nao wameufunga ufunuo, kana kwamba mpaka wakati wa Hadhrat Masihi tu watu walihitaji kushuhudia

kwa kujipatia busara na maarifa yao binafsi lakini vizazi vya baadaye ni vyenye bahati mbaya hata kwamba vimenyimwa funuo hizo kwa kudumu; ilhali mwanadamu daima anahitaji kushuhudia kwa macho matukio na busara ya binafsi. Dini inaweza kubaki kielimu mpaka pale tu ambapo sifa za Mwenyezi Mungu zinaendelea kudhihiri upya kila mara, waila hufa haraka ikibaki kama visa tu. Je dhamiri ya mtu inaweza kukubali kushindwa huku. Kama tunahisi nafsini mwetu kuwa tunahitaji kupata maarifa kamili ambayo hayawezi kutimilika bila maongezi na Mungu na ishara kubwa kubwa, basi rehema ya Mwenyezi Mungu yawezaje kutufungia mlango wa funuo? Je, katika zama hizi mioyo yetu imebadilika kuwa mingine au Mungu Amebadilika kuwa mwingine? Sisi tumeamini na kukubali kuwa katika zama moja ufunuo wa mtu mmoja unaweza kutilia nguvu maarifa ya malaki ya watu na hailazimu kila mtu afunuliwe ufunuo. Lakini hatuwezi kukubali kuwa ufunuo uondolewe moja kwa moja, na mikononi mwetu tuwe na visa tu ambavyo hatukuviona kwa macho yetu. Ni dhahiri kuwa jambo moja likiendelea kusimuliwa kama visa kwa mamia ya miaka bila kuwepo mfano wowote mpya wa kulisadikisha, hapo watu wenye tabia za

kifalsafa hawawezi kukikubali kisa hicho bila dalili madhubuti, hasa pale ambapo visa hivyo viwe na mambo yaonekanayo katika zama zetu kwamba hayawezekani. Ndiyo maana baada ya muda fulani watu wenye tabia ya kifalsafa wameendelea kuidhihaki miujiza kama hiyo na hawaishii kuishuku tu, na hii ni haki yao pia, kwani hufikiria mioyoni kuwa kama Mungu ni yule yule na sifa ni zile zile na mahitaji yetu ndiyo yale yale, kwa nini, basi, utaratibu wa ufunuo umekoma, ilhali roho zote zinapiga kelele kuwa sisi nasi tunahitaji utambuzi mpya. Ndiyo sababu, miongoni mwa Mabaniani malaki ya watu wakawa madaharia[17]. Kwani, Mapandit[18] wamewafundisha kuwa tangu mamilioni ya miaka utaratibu wa kufunuliwa na kuongea na Mungu umefungwa. Ndipo wakaingiwa na wasiwasi moyoni kuwa zama zetu zilihitaji sana funuo mpya za Mungu kuliko zama za Veda. Kama ufunuo ni ukweli hasa, kwa nini utaratibu huu haukudumu baada ya Veda? Ndiyo maana nchini India udaharia ukaenea sana. Ndiyo sababu miongoni mwa Mabaniani mtakuta mamia ya

[17] Wamkanao Mungu — Mwenezi.

[18] Viongozi wa dini ya Mabaniani — Mwenezi.

madhehebu yanayoidhihaki Veda na kuikataa. Miongoni mwao limo dhehebu la Jaini, na kwa kweli hata kundi la Masingasinga nalo lilitengana na Ubaniani kwa sababu ya fikara hizo. Kwani, kwanza katika dini ya Kibaniani mamia ya vitu vimeshirikishwa na Mungu, na lipo lundo kubwa la ushirikina ambamo Mungu hajulikani katu, tena madai ya Veda kufunuliwa na Mungu ni kisa tu kisichokuwa na uthibitisho wowote kinachoelezwa tangu malaki ya miaka, hakuna uhakikisho mpya. Ndiyo maana, Masingasinga halisi hawakiamini kitabu cha Veda. Hivyo, katika gazeti la Akhbare Aam linalotolewa Lahore, la tarehe 26 Septemba 1898, makala ya Singasinga mmoja yamechapishwa kuhusu suala hilo, na ameelezea kuwa kundi la Masingasinga haliamini Veda; wameagizwa na Maguru[19] kuwa kamwe wasiamini Veda. Ameandika nyimbo za Garanth[20] zinazomaanisha msiiamini Veda katu. Na ametangaza kuwa sisi kamwe sio wafuasi wa Veda wala hatuikubali kabisa. Naam, yeye hakukiri kuifuata Kurani Tukufu pia. Lakini sababu yake ni kuwa Masingasinga hawaijui

[19] Viongozi wa kiroho wa Masingasinga — Mwenezi.
[20] Kitabu kitakatifu cha Masingasinga — Mwenezi.

Islam, na hawana habri ya ile nuru Aliyoweka Mungu Mweza Mhifadhi wa milele katika Islam, na kwa sababu ya chuki ya kutoijua Islamu hawazitambui nuru zilizojaa ndani ya Kurani Tukufu. Bali kadri wanavyohusiana na Mabaniani kitaifa, hawahusiani na Waislamu; waila iliwatosha kuufuata wasia aliouandika Baba Nanak Sahib katika kanzu yake. Kwani, Baba Nanak alikwishaandika kwenye kanzu kuwa mbali na Islam hakuna dini iliyo sahihi na ya kweli. Basi, kuupoteza wasia huu muhimu wa mtawa kama huyo yasikitisha. Mkononi mwa Masingasinga mna kanzu tu pekee iliyo kumbukumbu ya maandiko ya mikono ya Bwana Baba Nanak. Na nyimbo za Granth zimekusanywa baadaye sana ambamo wachunguzi wana shaka nyingi. Mungu tu ndiye Anayejua kuwa mabadiliko gani yalifanywa ndani yake, na ni makusanyo ya watu gani. Lakini haipasi kisa hiki kielezwe hapa. Lengo letu ni hili kuwa kwa ajili ya kuimarisha imani za watu daima funuo mpya zinahitajika. Na funuo hizo zinatambulika kwa nguvu yenye madaraka, kwani minghairi ya Mwenyezi Mungu, nguvu yenye madaraka hanayo shetani, jini na afriti yeyote. Na kwa ufunuo wa Imamu wa zama usahihi wa funuo zingine

unathibitika.

Tumekwisha eleza kuwa Imamu wa zama anayo nguvu ya Uimamu katika tabia yake ya asili, na Mungu Huwa Amemjalia sifa ya uongozi. Na hii ni desturi ya Mwenyezi Mungu kuwa hataki kuacha watu katika hali ya kufarakana. Bali, kama ambavyo Akiingiza nyota nyingi katika mfumo wa Jua, Akalifanya Jua kuwa mfalme wao, ndivyo ambavyo Akiwapatia waumini wa kawaida nuru kama nyota sawa na daraja zao Akamfanya Imamu wa zama kuwa Jua lao. Na desturi hii ya Mungu inapatikana katika viumbe vyake sana hata kwamba baina ya nyuki pia nidhamu hii ipo kuwa kati yao pia huwa 'Imamu' aitwaye Ya'subu[21]. Na ndivyo alivyokusudia Mwenyezi Mungu kwa ufalme wa dunia kwamba awepo amiri na mfalme katika taifa. Na laana ya Mungu iwe juu ya wale wanaopenda mfarakano na hawafuati maagizo ya Amiri mmoja, ilhali Mungu mwenye shani tukufu Amesema kuwa:

أَطِيعُوا اللهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ[22]

Ulil-amri muradi wake kidunia ni mfalme, na

[21] Nyuki dume — Mwenezi.

[22] Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka kati yenu. An-Nisaa, 4:60

kiroho ni Imam wa zama. Na kimwili mtu yule asiyekuwa mpinzani wa malengo yetu na ambaye twaweza kunufaika naye kidini huyo anatokana nasi. Kwa hiyo nawasihi wanajumuiya wangu kuwa wauchukulie ufalme wa Waingereza kuwa miongoni mwa ulil-amri, nao wawatii kwa ukweli wa moyo, kwani hawatuzuii kutekeleza shughuli zetu za kidini, bali kutokana na kuwepo kwao sisi tumepata utulivu mkubwa, na tutakuwa tunafanya hiyana tusipokiri kuwa Waingereza wameisaidia dini yetu kwa namna fulani ambayo hata wafalme wa Kiislamu wa India hawakuweza kujaliwa. Kwani baadhi ya wafalme wa Kiislamu wa India kwa sababu ya ulegevu wao waliutelekeza mkoa wa Panjab na kutokana na uzembe wao huo sisi pamoja na dini yetu tulipata taabu nyingi katika zama za serikali mbalimbali za Kisingasinga, hata ikawa vigumu kusali sala za jamaa misikitini na kutoa adhana kwa sauti kubwa. Na mkoani Panjab Uislamu ulikuwa umekufa. Kisha wakaja Waingereza — bali na bahati zetu nzuri ziliturejea — nao wakaihami dini ya Kiislamu, na wakatupatia uhuru kamili kwa kutekeleza faradhi zetu za dini. Na misikiti yetu ikafunguliwa, na ndipo baada ya muda mrefu alama za Kiislamu zikaanza kuonekana. Je hisani hii haipaswi

ikumbukwe? Bali, ukweli ndio huu kwamba baadhi ya wafalme wa Kiislamu wasiokuwa na bidii wakatusukumia ndani ya shimo la ukafiri kwa uzembe wao na Waingereza wakatushika mkono na kututoa nje tena. Hivyo, kupika majungu kwa kuleta uasi dhidi ya Waingereza ni kuzisahau neema za Mwenyezi Mungu.

Kisha nikirejea kwenye mada yetu nasema kuwa jinsi Kurani Tukufu ilivyoagiza kwa mkazo khusu utamaduni wa kimwili kuwa tuishi chini ya mfalme mmoja, ndivyo ulivyo mkazo huo huo kwa utamaduni wa kiroho pia, na ndiko Anakoashiria Mwenyezi Mungu katika dua hii Anayotufundisha kuwa:

اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ ۙ﴿٦﴾
صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ ۙ[23]

Hivyo basi, yapasa kuzingatia kuwa ingawaje hakuna muumini, bali mwanadamu, bali hata mnyama yeyote asiyejaliwa neema za Mwenyezi Mungu lakini hatuwezi kusema kwamba Mwenyezi Mungu Ametoa agizo hili ili kuwafuata hao. Hivyo, aya hii yamaanisha kuwa watu ambao

[23] Tuongoze njia iliyonyooka. Njia ya wale Uliowaneemesha. Al-Faatiha: 1:6,7

wamenyeshewa mvua ya neema za kiroho kikamilifu na kitimilifu utujaalie njia zao ili tuzifuate. Basi, katika aya hii kuna ishara hii tu kwamba nyinyi muwe pamoja na Imamu wa zama.

Ikumbukwe kuwa katika neno Imamu wa zama, wanaingia Nabii, Rasuli, Muhaddathi na Mujaddidi kwa jumla; lakini watu ambao hawajaamrishwa kuwaongoza viumbe wa Mungu wala hawajajaliwa sifa hizo kamilifu, watu hao hata wakiwa mawalii au watawa sana hawawezi kuitwa ni Imamu wa zama.

Sasa mwishoni swali hili linabakia kuwa katika zama hizi Imam wa zama ni nani ambaye Waislamu wa kawaida na watawa na waotaji njozi na wapokeaji wa funuo wote hao wamelazimishwa na Mwenyezi Mungu kumfuata? Basi nasema wakati huu bila hofu yoyote kuwa kwa fadhili na hisani za Mwenyezi Mungu

## Mimi ndimi Imamu wa zama

na ndani yangu Mwenyezi Mungu Amejumuisha alama na masharti yote hayo na Amenituma mwanzoni mwa karne hii ambamo miaka kumi na mitano tayari imeshapita. Na nimedhihiri katika

wakati ambapo itikadi za Kiislamu zilijaa hitilafu, na hakuna itikadi isiyokuwa na hitilafu. Kadhalika fikara isiyokuwa sawa kabisa kuhusu kushuka kwa Masihi ilikuwa imeenea; na katika itikadi hii pia hali ya hitilafu ilikuwa kwamba baadhi yao waliamini Hadhrat Isa[as] yuko hai, na wengine waliamini amekwisha fariki; baadhi yao waliamini kwamba atashuka kimwili na wengine walikuwa na itikadi atashuka Kiburuzi[24]. Baadhi yao wakaamini atashuka Dimashki na wengine katika Makka, wengine katika Baitul Muqaddas na wengine ndani ya Jeshi la Kiislamu, na wengine walidhania kuwa atashuka katika India. Basi, rai hizo na kauli hizo zote zilizotofautiana zilimhitaji mwamuzi wa kutoa hukumu. Basi, Mwamuzi huyo ni mimi. Mimi nimetumwa kuja kuvunja kiroho msalaba na kuondoa hitilafu. Mambo hayo mawili yalihitaji kuwa mimi nitumwe. Haikunilazimu nitoe uthibitisho mwingine wa ukweli wangu, kwani haja yenyewe ni dalili tosha. Lakini, hata hivyo Mwenyezi Mungu Amedhihirisha ishara nyingi za kunisaidia. Nami kama nilivyo Mwamuzi wa kuamua hitilafu

---

[24] “Kibaruzi” humaanisha mtu mwingine atatokea mfano wa Nabii Isa[as]. — Mwenezi.

nyingine, ndivyo nilivyo Mwamuzi katika swala la kifo au uhai wa Masihi. Na ninaamua kuwa kauli ya Imam Malik na Ibn Hazm na Mu‘tazila juu ya kifo cha Masihi[as] ni sahihi na nawaona Masunni wengine wamekosea katika hili. Basi mimi nikiwa Mwamuzi ninatoa hukumu baina ya wabishanaji hao kwamba katika kauli ya ushukaji kundi hili la Masunni ni sahihi, maana ushukaji wa Masihi kiburuzi ulikuwa ni lazima. Naam, walikosea katika kueleza namna ya kushuka kwake. Ushukaji ulikuwa wa kiburuzi, sio wa kimwili. Na katika swala la kifo cha Masihi[as] msimamo wa Mu‘tazila na Imam Malik na Ibni Hazm na wataalamu wenzao ni wa kweli, kwani kwa mujibu wa andiko wazi la Kurani Tukufu, yaani aya[25] فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي, ilikuwa hakuna budi Masihi afariki kabla Wakristo hawajaharibika. Huu ni uamuzi kutoka kwangu mimi nikiwa Mwamuzi. Sasa mtu anayeukataa uamuzi wangu, anamkataa Yule Aliyenifanya kuwa Mwamuzi. Kama niulizwe swali kuwa kuna uthibitisho gani kwamba u mwamuzi, basi, jibu lake ni kuwa zama zenyewe alimotakiwa Mwamuzi aje, zipo hizi, na kaumu ambayo Mwamuzi alitakiwa kurekebisha

---

[25] Lakini Uliponifisha. Al-Maaida, 5:118

makosa yake ya itikadi ya kimsalaba kaumu hii ipo, na ishara zilizotakiwa kutoa ushahidi juu ya Mwamuzi huyo, ishara hizo zimekwisha dhihirika, na hata sasa ishara zinaendelea kutokea. Mbingu inadhihirisha ishara, ardhi pia inadhihirisha ishara. Na wamebarikiwa wale ambao macho yao sasa yasiwe yamefumbika.

Mimi sisemi kuwa muamini tu ishara zilizokwishatokea, bali nasema kuwa kama mimi siye Mwamuzi, basi shindaneni nami katika ishara nilizoonyesha. Dhidi yangu niliyekuja wakati wa hitilafu nyingi za kiitikadi mahojiano yote ni bure tu. Kila mtu ana haki ya kuongelea juu ya Mwamuzi tu, nami nimeisha timiza hiyo. Mungu Amenipa ishara nne:

1. Mimi nimejaliwa mwujiza wa ujuzi na ufasaha wa lugha ya Kiarabu ulio kama kivuli cha Kurani Tukufu, hakuna yeyote anayeweza kuukabili.

2. Mimi nimepewa ishara ya kufafanua kweli za Kurani Tukufu na maarifa yake; hakuna yeyote anayeweza kushindana nami katika hilo.

3. Mimi nimepewa ishara ya kupokelewa maombi kwa wingi sana, hakuna yeyote wa kushindana nami katika hilo. Naweza kusema kwa kuapa kuwa dua zangu karibu thelathini elfu zimeisha

kubaliwa na ushahidi wake ninao.

4. Mimi nimepewa ishara za habari za ghaibu, hakuna yeyote anayeweza kushindana nami kwa hilo. Shuhuda hizi za Mwenyezi Mungu ninazo na bishara za Mtume wa Mungu[saw] zimetimia kwa ajili yangu kama ishara zing’aazo.

آسماں بارد نشان الوقت مے گوید زمیں

این دو شاہد از پئے تصدیق من استادہ اند

Mbingu inamimina ishara, ardhi yasema wakati ni huu huu; hizo mbili ni mashahidi waliosimama kunisadikisha.

Muda umepita jua na mwezi vilipatwa ndani ya mwezi wa Ramadhani, hija ikasimamishwa, na kwa mujibu wa Hadithi tauni pia ikaenea nchini, na ishara nyingi zikadhihirika kwa mkono wangu ambazo mamia ya Mabaniani na Waislamu ni mashahidi wake, ambazo sikuzitaja. Kwa sababu hizi zote, mimi ni Imamu wa zama. Na Mungu Ananisaidia, naye Amesimama kwa ajili yangu kama  upanga mkali, na nimepashwa habari kwamba yeyote atakayesimama dhidi yangu kwa ukorofi atadhalilishwa na kufedheheshwa. Angalieni, nimekwisha fikisha agizo lililokuwa jukumu langu. Na mambo haya nimekwisha andika mara nyingi katika vitabu vyangu. Lakini

tukio lililonihimiza niandike tena mambo haya ni kosa la kijitihadi la rafiki yangu ambalo baada ya kulijua nimeandika kijitabu hiki kwa moyo wenye uchungu sana. Maelezo ya tukio hili ni kuwa katika siku hizi hizi yaani katika mwezi Septemba 1898 ambao ndio mwezi wa Jumada I 1316 hijria, rafiki yangu mmoja ninayemfahamu kuwa ni mtu asiyekuwa na madhara, mwema, mcha-Mungu na mtawa na ambaye tangu awali kuhusuye nina dhana njema sana — Mungu ndiye Mwenye kumhesabia — lakini naona ameangukia kosa katika baadhi ya fikira na kutokana na kosa hili namhofia pia. Yeye akaniwasilia Qadian kwa kupata shida za safari na kwa kumchukua pamoja naye rafiki yangu mmoja mpendwa. Yeye akanisimulia funuo zake nyingi. Mimi nikafurahi sana kuwa Mwenyezi Mungu Amempa heshima ya kufunuliwa. Lakini katika mfululizo wa funuo akanisimulia ndoto yake moja hii pia kwamba alisema katika ndoto kunihusu mimi kuwa kwa nini mimi nifanye baiat yake, bali yeye apaswa afanye baiat yangu. Kutokana na ndoto hii ilijulikana kuwa yeye haniamini kuwa Masihi Mau‘udi, na kwamba yeye hana habari ya masaala ya Uimamu wa kweli. Hivyo basi, huruma yangu imenitaka nimwandikie kijitabu hiki kwa

kubainisha Uimamu wa kweli, na kuandika hakika ya baiati. Basi, mimi nimeisha andika mengi ndani ya kijitabu hiki kuhusu Imamu wa kweli mwenye haki ya kuchukua baiati. Iliyobaki ni hakika ya baiati. Nayo ni hii kuwa neno baiati limetokana na neno Bai‘, na Bai‘ ni makubaliano ya kutoa kitu kimoja badala ya kitu kingine. Basi, shabaha ya baiati ni hii kuwa anayefanya baiati ajiuze nafsi yake pamoja na vyote vilivyoilazimu, kwa mwongozi mmoja ili badala yake ajipatie elimu ya kweli na baraka kamilifu ambazo zisababishe kupata maarifa na ukombozi na radhi ya Mwenyezi Mungu. Ni dhahiri kwa hiyo kuwa baiati haimaanishi toba pekee, kwani toba kama hii mtu anaweza kujifanyia hata mwenyewe. Bali inakusudiwa maarifa na baraka na ishara zile zinazovutia kwenye toba ya kweli. Lengo hasa la baiati ni kuwa akijitupa nafsi yake katika utumishi wa mwongozi wake apate badala yake elimu na maarifa na baraka ambazo kwazo imani iimarike na maarifa iongezeke, yapatikane mahusiano safi na Mwenyezi Mungu. Na hivyo akitoka kutoka katika jahanamu ya kidunia aepukane na jahanamu ya akhera, na akipona upofu wa kidunia awe salama katika upofu wa akhera. Hivyo, kama kuna mtu wa kuweza kutoa matunda ya baiati,

itakuwa ni uovu wa hali ya juu kama yeyote ajitenge naye kwa kusudi.

Mpenzi wangu, sisi tuna njaa na kiu ya maarifa, kweli na baraka za kimbingu, na hata tukinywa bahari nzima hatuwezi kutosheka. Hivyo kama mtu anataka kutuchukua katika utumwa wake, basi kuna njia hii rahisi kuwa afanye biashara nasi kwa kuzingatia maana ya baiati na hekima yake hasa. Na kama anazo kweli maarifa na baraka za kimbinguni ambazo sisi hatujapewa, au awe amefunguliwa elimu za Kurani ambazo hatujafunguliwa, basi mtawa huyo kwa jina la Mungu Atuchukue katika utumwa na utii wake na atupatie maarifa ya kiroho, elimu za ndani za Kurani na baraka za kimbingu. Mimi sitaki kuleta usumbufu zaidi, jamaa yetu anayepata funuo aeleze tu elimu ya ndani na maarifa ya sura Ikhlas katika mkutano, na kama tusiweze kueleza mara elfu zaidi kuliko yake, basi nitakuwa mtiifu wake.

ندارد کسے باتو ناگفتہ کار

و لیکن چو گفتی دلیلش بیار

Kama hukusema kitu, hakuna mtu anayehusika nawe; lakini kama umesema kitu, basi lete uthibitisho wake.

Kwa vyovyote, kama unazo kweli na maarifa na

baraka zenye athari ya kimwujiza ndani yake, basi si mimi tu bali wanajumuiya wangu wote watafanya baiati kwako, na atakuwa mkorofi sana asiyefanya hivyo. Lakini mimi nisemeje na niandikeje. Ninasema nikiomba msamaha kuwa niliposikia funuo zako zilizokuwa zimeandikwa, nikakuta katika baadhi ya sehemu makosa ya sarufi na sintaksia. Tafadhali, usikasirike, hiyo pia nimeeleza kwa nia njema na upole na kama nasaha za kidini. Hata hivyo kwa maoni yangu, kama katika maneno ya funuo za watu wasiojua na wasioweza kusoma na kuandika kutokee makosa ya sarufi na sintaksi, hapo ufunuo wenyewe hauwezi kupingwa. Hili ni jambo jepesi sana na linahitaji maelezo marefu ambapo hapa sio mahali pake. Akihamaki kwa kusikia makosa kama hayo, ana udhuru, kwani hana habari ya hekima ya kiroho. Lakini ufunuo huo unahesabiwa wa daraja ya chini ambao haung'ari kikamilifu kwa nuru ya Mwenyezi Mungu. Kwani, ufunuo huwa wa daraja tatu: ya chini, ya wasitani na ya juu. Kwa vyovyote mimi nimesikitishwa na makosa hayo, nikaomba moyoni dua kuwa rafiki yangu mheshimiwa asipate kumweleza sheikh yeyote mkorofi mwenye mtazamo finyu funuo hizi ambazo

kidhahiri zaweza kupingwa, kwani huyo atamcheka na kumfanyia dhihaka bure tu. Ufunuo usio na elimu ya ndani na maarifa na uliojaa makosa pia hauwezi kumfaidisha yeyote, rafiki au mpinzani, hasa katika zama hizi; bali badala ya faida kuna hofu ya kuleta hasara. Kwa imani na ukweli nasema kwa kuapa kuwa jambo hili ni kweli kabisa. Rafiki yangu mpendwa atasogelea zaidi kwa Mwenyezi Mungu[26] kadri utakavyozidi usafi wa moyo. Hii ndiyo siri kuwa wahyi wa Kurani unapita sana wahyi wa manabii wengine katika ufasaha na balagha pia zaidi ya kupita katika elimu ya ndani. Kwani, Mtume wetu[saw] alijaliwa usafi wa moyo zaidi kuliko wote. Basi, wahyi huo kwa kimaana ukadhihirika kwa sura ya elimu ya ndani na kimaneno ukadhihiri kwa sura ya ufasaha na balagha. Rafiki yangu azingatie hii pia kwamba, kama nilivyoeleza, baiati ni kama kuuza na kununua. Nami nasema kwa kuapa kuwa kadri rafiki yangu mwanachuo Maulawii Abdul Karim wakati wa kutoa mawaidha anavyoeleza elimu za ndani za Kurani Tukufu, mimi situmaini kuwa hata sehemu yake ya elfu moja inaweza

[26] Nina yakini kwamba kama rafiki huyu mheshimiwa akielekea kwa Mungu zaidi, funuo zake zitaboresheka. Mwandishi.

kuelezwa na rafiki yangu huyu. Sababu yake ni kuwa upande wa kufunuliwa bado una kasoro na upande wa kutia bidii hamna kabisa; haijulekani kuwa mpaka sasa amepata fursa hata ya kusikia Kurani Tukufu kutoka kwa mhakiki yeyote au hapana.[27] Kwa ajili ya Mungu usikasirike, mpaka sasa hujaelewa uhakika wa baiati kuwa katika hiyo watoa nini na wapata nini. Katika Jumuiya yangu na katika waja wa Mungu waliofanya baiati yangu kuna mtu mmoja mwanachuo mwenye shani kubwa, naye ndiye Maulawii Tabibu, Hafidh, Alhajj Nuruddini ambaye kana kwamba anavyo vitabu vyote vya maelezo ya Kurani Tukufu vinavyopatikana duniani. Kadhalika moyoni mwake mna hazina ya elimu ya ndani ya Kurani. Kama wewe kweli umepewa heshima ya kupokea baiati, basi umfundishe yeye juzuu moja

[27] Sikatai kuwa chemchemi za elimu iliyojaliwa na Mungu zifunguliwe kwako. Lakini mpaka sasa bado. Njozi na kashfi huwa na istiara na majazi sana, lakini wewe umeichukulia njozi yako kidhahiri. Bwana Mujadidi Sarhindi aliona katika kashfi moja kwamba Mtume Mtukufu[saw] alipata cheo cha Khalilullahi kumpitia yeye. Na Shah Waliyyullahi akampita na akaona kana kwamba Mtume Mtukufu[saw] amefanya baiati kwa mkono wake. Lakini kwa sababu ya upana wa elimu yao hawakufikiria kama ulivyofikiria wewe, bali akaifumbua. Mwandishi.

tu ya Kurani pamoja na elemu ya ndani na maarifa. Watu hawa sio wendawazimu kwamba wamefanya baiati kwangu tu na kuwaacha wale wengine wafunuliwao. Kama wewe ungemfuata Hadhrat Maulawii Sahib ingekuwa afadhali. Hebu, fikiria kwamba msomi huyo ambaye akiacha makazi yake akaja kukaa kwangu, na kusumbuka akiishi katika vyumba vya matope, anavumilia taabu hivi hivi bila kuona kitu? Mpenzi na rafiki yangu afunuliwaye ufunuo azingatie k

ao huo wa kimwujiza achukue baiati ya mpenzi wa Kurani Tukufu kama Nuruddini, hapo mimi na Jumuiya yangu itajitolea kwako. Je, kwa sentensi chache za ufunuo zisizotambulikana ambazo nazo si sahihi mara nyingi, daraja hii inaweza kupatikana kwamba mtu ajifikirie kuwa Imamu wa zama? Ndugu yangu, kwa Imamu wa zama kuna masharti mengi sana ndipo aweza kuikabili dunia nzima.

هزار نکتهٔ باریک تر زمو اینجاست
نه هرکه سر بتراشد قلندری داند

Hapa pana mambo elfu ya busara yaliyo membamba zaidi kuliko unywele, Siyo kwamba kila ajinyoaye kichwa autambua Ukalandari.[28]

Ndugu yangu anayefunuliwa ufunuo asiwe amedanganyika kwamba yeye anashukiwa sana na maneno ya ufunuo. Mimi nasema kweli kabisa kuwa ndani ya Jumuiya yangu kuna wengi sana wanaofunuliwa kama huyu hata kwamba funuo za baadhi yao ziko kiasi cha kitabu kizima. Sayyid Amir Ali Shah kila wiki ananiletea karatasi nzima zinazoandikwa funuo zake — na wapo baadhi ya akina mama wanaonisadikisha ambao hawakusoma hata neno moja la Kiarabu lakini wanafunuliwa kwa Kiarabu — nashangaa sana kwamba katika funuo zake makosa huwa machache kuliko funuo zako. Tarehe 28 Septemba 1898, funuo zake chache nilipokea katika barua ya ndugu yake Fateh Muhammad Buzdar. Kadhalika wapo wapokeaji funuo wengi katika Jumuiya yangu, mmojawapo anakaa hata mjini Lahore. Lakini je, kwa funuo kama hizo mtu anaweza asijali kufanya baiati kwa Imamu wa zama? Mimi

---

[28] Ma-Kalandari ndio wanaotengana na mambo yote, alama yao maalumu ni vichwa vyao vilivyonyelewa daima, wanahesabiwa kuwa madaruweshi. — Mwenezi.

sina udhuru wa kufanya baiati kwa yeyote, lakini shabaha ya baiati ni kutoa elimu za kiroho na kuimarisha imani. Sasa nieleze kwamba wewe katika baiati yako utafundisha elimu gani na utaeleza maana gani za ndani za elimu ya Kurani Tukufu. Karibu, tafadhali, utuonyeshe nguvu za Uimamu na sisi sote tutafanya baiati.

حضرتِ ناصح گر آئیں دیدہ و دل فرشِ راہ
پر کوئی مجھ کو تو سمجھائے کہ سمجھائیں گے کیا

Kama mtoa mwaidha akija, nitampokea kwa moyo mkunjufu. Lakini anifahamishe mtu kwamba bwana huyo atanifahamishaje!!

Nikipiga ngoma nasema kuwa chochote Alichonijalia Mungu, ndicho alama ya Uimamu. Mtu aonyeshaye alama hiyo ya Uimamu na athibitishe kuwa amenizidi katika ubora, mimi nipo tayari kufanya baiati kwake. Lakini hakuna mabadiliko katika ahadi za Mungu, hakuna anayeweza kushindana naye. Miaka ishirini takribani iliyopita, katika Barahin-i-Ahamadiyya ufuno huu mmeandikwa:

اَلرَّحْمٰنُ عَلَّمَ الْقُرْآنَ ۔ لِتُنْذِرَ قَوْمًا مَا اُنْذِرَ آبَاؤُ هُمْ

وَلِتَسْتَبِيْنَ سَبِيْلُ الْمُجْرِمِيْنَ قُلْ اِنِّىْ اُمِرْتُ وَ اَنَا اَوَّلُ الْمُؤْمِنِيْنَ[29]

Sawa na ufunuo huu, Mungu Amenijalia elimu za Kurani na Ameniita jina mwaminio wa kwanza na Akanijaza maarifa na elimu za ndani kama bahari. Na mara kwa mara Akanifunulia ufunuo kwamba katika zama hizi hakuna utambuzi wa Mungu wala upendo wa Mungu ulio sawa na utambuzi wako na upendo wako. Basi, Wallahi, mimi nimejitokeza katika uwanja wa mashindano ya mwereka. Asiyenikubali, hivi karibuni baada ya kufa atafedheheka, naye sasa yuko chini ya hoja ya Mungu. Ewe ndugu! kazi yoyote iwe ya dini au ya dunia haiwezi kufanyika bila kuwa na ustadi. Nakumbuka kwamba ofisa fulani Mwingereza aliletewa mtu mmoja wa ukoo mkubwa ili ateuliwe kuwa mkuu wa tarafa. Lakini huyo aliyepelekwa alikuwa hajui kitu, hata hakujua Kiurdu. Yule Mwingereza akasema mimi nikimfanya mkuu wa tarafa, ni nani atakayeamua kesi badala yake? Siwezi kumpa kazi yoyote isipokuwa asaidie kukusanya ushuru na apewe

[29] Tafsiri: “Mwingi wa Rehema Amefundisha Kurani, ili uwaonye watu ambao hawakuonywa baba zao, na ili njia ya wakosefu ibainike. Sema, mimi nimeamriwa, na mimi ni wa kwanza wa wanaoamini.”

usaidizi wa rupia tano tu sio mshahara. Kadhalika Mwenyezi Mungu naye Anasema:

اَللّٰهُ اَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهٗ [30]

Je, yule ambaye maelfu ya maadui na marafiki wanamjia wakimletea maswali na hoja za upinzani, naye amejaliwa unaibu wa Nabii, yampasa kuwa na shani yake kwamba awe na sentensi tu chache za ufunuo ambazo nazo hazina hata ushahidi. Je wafuasi wake na wapinzani wake wanaweza kupata utulivu wowote kwake?

Sasa nataka kumaliza mada hii, kama humo kuna neno lolote la kuchukiza ndani yake basi namwomba radhi kila mtu pamoja na rafiki yangu mpokeaji wa funuo, maana kwa nia njema nimeandika mistari hii michache, nami nampenda sana ndugu yangu huyu kwa moyo na ninaomba kuwa Mungu Awe pamoja naye. Basi.

Ndimi,

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian

Wilaya ya Gurdaspur.

---

[30] Mwenyezi Mungu ndiye Ajuaye zaidi Atakapoweka ujumbe wake. (Al-An□aam, 6:125)

## Barua ya Maulawii Abdul Karim kwa rafiki yake mmoja[31]

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [32]

اَلْحَمْدُ لِوَلِيِّهٖ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى نَبِيِّهٖ [33]

Ama baadu

Kutoka kwa Abdul Karim kwa ndugu yangu na mpendwa wangu Nasrullah Khan.

سَلَامٌ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللّٰهِ وَبَرَكَاتُهٗ [34]

Leo mara nyingine moyo wangu umepata kuvutika kukusimulia habari za machungu ya moyo wangu, huenda nawe ukawa wanihurumia. Kuvutika huku baada ya muda mrefu hakuwezi kukosa masilahi. Mhamasishaji wa mioyo huwa Hawaelekezi waja wake kutenda kazi bure.

---

[31] Niliona mara barua aliyoiandika ndugu yangu Maulawii Abdul Karim kwa rafiki yake mmoja. Basi, kwa munasaba yake fulani na madhumuni ya kijitabu hiki niliichapisha. — Mwandishi.

[32] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[33] Sifa zote njema zamhusu Mungu, sala na salamu ziwe juu ya Nabii wake[saw].

[34] Salam ziwe kwenu na Rehema za Mungu pamoja na baraka zake.

Bwana Chaudhry, mimi nami ni mwanadamu, nimetokea ndani ya tumbo la mwanamke dhaifu. Hakuna budi niwe na udhaifu wa kibinadamu, mvutano wa mahusiano na uzito ndani yangu pia. Aliyetoka tumboni mwa mwanamke, kama hana matatizo mengine hawezi kuwa na moyo mgumu. Yupo hai mama yangu mzee mwenye moyo wa huruma, mgonjwa wa kudumu. Na baba yangu pia yupo. (Ewe Mwenyezi  Mungu mpe afya na msaidie na mjaalie mema). Ninao ndugu zangu pia, ndugu wapendwa sana. Ninao wengine pia ninaohusiana nao. Sasa, je, mimi nina moyo mgumu kama jiwe ambaye miezi mingi imepita ninaendelea kujikalia hapa; au je, nina kichaa na hisia zangu zimevurugika; au je, mimi ni mfuasi mbumbumbu na sina ujuzi kabisa wa elimu za kweli; au je, mimi ni mtu ninayejulikana ndani ya jamii yangu, mtaa wangu na mji wangu kwa kuishi maisha ya kifuska; au je, mimi ni muflisi na ni maskini hohehahe ninayejigeuza-geuza sura ili nipate chakula cha kutia tumboni? Mungu Anajua na malaika wanashuhudia kuwa kwa msaada wa Mungu nimeepukana na aibu zote hizo. Mimi sijitakasi nafsi yangu, bali Mungu Humtukuza Amtakaye.

Basi ni kitu gani kilichozalisha uimara ndani

yangu ulioyashinda mahusiano yote hayo? Ni jambo wazi sana na linaishia kwenye neno moja tu, nalo ndilo “utambuzi wa Imamu wa zama”. Allah, Allah! Ni jambo gani hili ambamo mna nguvu kubwa inayovunjilia mbali mahusiano yote. Wajua vizuri kuwa mimi ninaelewa sawa na uwezo wangu elimu za ndani na siri za kitabu cha Mungu. Na nyumbani mwangu sina shughuli nyingine zaidi ya kusoma na kusomesha kitabu cha Mungu. Basi, najifunza nini hapa? Je, kusoma huku nyumbani na kuwa maarufu katika jamaati kubwa na kuwa lengo la macho ya watu, hayo yote hayatoshi kuibembeleza roho yangu na nafsi yangu? Hayatoshi kabisa. Wallahi tena Wallahi hayatoshi katu. Mimi nilikuwa nasoma Kurani Tukufu na kuwasomea watu, nikisimama kwenye mimbari siku ya Ijuma, nikatoa mawaidha yenye athari kubwa juu ya khulka njema na kuwaonya watu kwa adhabu ya Mungu na kuwasisitizia waepukane na mambo yaliyokatazwa; lakini daima nafsi yangu ndani kwa ndani ikanilaumu kwamba:

لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ۝۳
كَبُرَ مَقْتًا عِندَ اللَّهِ أَن تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ۝۴ [35]

---

[35] Mbona mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele

Nikawaliza wengine lakini mwenyewe sikulia. Nikawazuia wengine wajiepushe na mambo yasiyofaa kutendwa na kusemwa, lakini mwenyewe sikujizuia. Kwa kuwa sikuwa mshaufu makusudi wala mchoyo wala mdanganyifu, wala shabaha ya bidii yangu haikuwa kupata heshima wala dunia, basi kila nilipokuwa peke yangu mawazo hayo yakanijia kwa kishindo. Lakini kwa vile nilikuwa sioni njia yoyote ya kujirekebisha, na imani haikuniruhusu kuridhika na matendo makavu ya uongo, hatimaye kutokana na misukosuko hii, nilishikwa na maradhi kali ya moyo kudhoofika. Mara nyinngi nilifunga nia ya kuacha kabisa kusoma, kusomesha na kutoa mawaidha, lakini tena kwa hamu sana nikasoma vitabu juu ya khulka, vitabu vya usufii na maelezo ya Kurani. Nikasoma Ihyaul‘ulum, Awariful maarif, jalada zote nne za Futuuhaati Makkiyyah na vitabu vingine vingi na nikavisoma kwa makini sana. Na Kurani Tukufu ilikuwa ni chakula cha roho yangu, na alhamdu-lillahi ndivyo ilivyo hata sasa. Tangu utotoni hata kabla sijajitambua ninao upendo mkubwa wa kitabu hiki kitakatifu hata kwamba siwezi kueleza hali na kiasi chake.

---

ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda. As-Saf, 61:3,4

Ilmuradi, elimu ikaongezeka na nikapata maneno mengi ya vichekesho kwa kufurahisha hafla na kwa kupamba waadhi. Na nikaona kuwa wagonjwa wengi wakapona kwa mikono yangu, lakini hayakupatikana mabadiliko yoyote ndani yangu. Hatimaye baada ya mashaka sana na wa kina ikabainika kwangu kwamba uchafu huu hautaondolewa bila kuwa na mfano ulio hai ama pasipo kufikia ile chemchem ya uzima iwezayo kuosha takataka za ndani. Mwongozi mkamilifu, Khatamul Ambiyaa, amani na rehema za Mungu ziwe juu yake, aliwafanyaje masahaba kupitia vituo mbalimbali katika safari ya kiroho kuelekea kwa Mungu katika miaka 23? Kurani ilikuwa ni elimu, naye yeye[saw] alikuwa mfano wake wa kweli kimatendo. Maneno matupu na maelezo ya kielimu hayakutilia moyoni heshima na enzi ya Kurani Tukufu; bali mifano ya kimatendo ya Mtume Mtukufu[saw] na khulka njema zisizo na kifani pamoja na misaada mingine ya kimbingu na kufululiza kudhihirika kwake kukatilia athari ya kudumu mioyoni mwa mahadimu wake. Kwa vile Islamu inapendwa sana na Mwenyezi Mungu, na Amependa kuidumisha mpaka mwisho wa dunia, hivyo hakupenda kuwa dini hii pia — kama dini zingine — ikibakia katika sura ya visa na hadithi

za kubuniwa ikawa kama kitu kisicho na thamani. Ndani ya dini hii tukufu waja walio mifano hai wameendelea kupatikana katika kila zama ambao kielimu na kimatendo waliwakumbusha watu zile zama za yule aliyeleta Kurani Tukufu, baraka za Rahmani zimfikie. Sawa na desturi hii Mwenyezi Mungu katika zama zetu hizi Amemwinua baina yetu Hadhrat Masihi Mau‘udi, Mwenyezi Mungu Amsaidie sana, ili yeye awe shahidi mmoja juu ya zama hizi. Niliyotaka kuandikia ndani ya barua hii yalikuwa ni dalili chache za kimaono juu ya haja ya kuwepo kwa Imamu huyu wa kweli, lakini wakati huo huo kwa kuhimizwa na baadhi ya sababu Hadhrat Mtukufu mwenyewe ameandika juzi kijitabu kidogo juu ya “Haja Ya Imamu” kitakachochapishwa hivi karibuni na kuenezwa, hivyo nimeacha nia hiyo.

Mwishoni, nakukumbusha vikao vyetu vilivyojaa wema na kuhudhuria kwako siku zote katika darasa la kitabu cha Mungu kwa itikadi njema na dhana yako njema kamilifu kunihusu mimi, na juu ya hayo yote matayarisho yako mema kwa moyo mwema. Nakusihi dhamira yako safi na tabia yako nyofu kwamba utafakari. Huu ndio wakati wa hatari sana. Iko wapi imani ile hai ambayo Kurani inataka na ule moto uunguzao dhambi ambao

Kurani Tukufu inataka kuzalisha vifuani mwa watu? Nakuhakikishia nikiapa. Kwa jina la Mungu mwenye Arshi kuu kuwa imani hiyo inapatikana kwa kufanya baiati kwa mkono wa naibu wa Rasuli, Masihi Mau‘udi, na kukaa pamoja naye huyu mtukufu. Sasa, ukichelewa kutenda jambo hili la kheri naogopa isije mabadiliko ya kuogofya yakazalika moyoni.

Ondoa hofu ya dunia, poteza kila kitu kwa ajili ya Mungu, kwa yakini utapata vyote.

Wassalam<br>
Ndimi mnyeyekevu Abdul Karim,<br>
kutoka Qadian, Octoba 1, 1898

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [36]

نَحْمَدُهٗ وَ نُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ [37]

## Kodi ya Mapato na Ishara Mpya

صدق را ہر دم مدد آید ز ربّ العٰلمین
صادقاں را دستِ حق باشد نہاں در آستیں
ہر بلا کز آسماں بر صادقے آید فرود
آخرش گردد نشانے از برائے طالبیں

Ukweli unasaidiwa kila saa toka kwa Mola wa walimwengu. Kwa wakweli, Mkono wa Mungu unafichikana ndani ya mkono wa kanzu yao.

Kila balaa inayomshukia mkweli kutoka mbinguni, hatimaye huwa ishara kwa watafutao haki.

Baadhi ya maadui zetu majahili walikuwa na huzuni na uchungu moyoni kwa sababu ya kushindwa kwao katika kesi ya Daktari Martin Clark. Kwani walipata kushindwa vibaya juu ya kufanya juhudi kubwa katika kesi ambayo

[36] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[37] Tunamhimidia yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

ingeathiri maisha na heshima yangu, na siyo kushindwa tu bali utabiri wa kiufunuo uliohusu kesi hii pia ulitimia ambao habari zake watu waaminifu na wenye heshima zaidi ya mia mbili walikuwa wamearifiwa, na ambao ulienezwa vizuri baina ya watu wote mapema sana. Lakini ni masikitiko kwamba kwa dhana mbaya na upapara wapinzani wakapata ushinde wa pili pia. Ni hivi kwamba kwa kuangalia kijuu-juu tu pasipo uchunguzi wa mahakama yoyote nikadaiwa rupia 187 na Anna 8 baada ya kukadiriwa kodi ya mapato yangu, hapo wale watu ambao hakuna haja ya kuandika majina yao (wenye akili wenyewe wataelewa) walifurahi sana mioyoni mwao, wakadhani kuwa kama tulikosa shabaha mara ya kwanza, basi afadhali fedheha ile imeondolewa kidogo katika kesi hii. Lakini haiyumkiniki kuwa watu wawatakiao wengine vibaya na wafutao tamaa ya nafsi wapate kushinda, kwani ushindi haupatikani kwa mipango ya mtu na kwa ujanja. Bali Yuko Mmoja Anayeangalia mioyo ya watu na huchambua mawazo yao ya ndani na hutoa hukumu kutoka mbinguni sawa na nia zao. Hivyo, hakuyafanya matakwa ya watu wenye fikira mbaya yatimie, na baada ya upelelezi kamili kodi ya mapato

ikasamehewa tarehe 17 Septemba 1898. Katika kufunguliwa kesi hii ilifichikana hekima moja hii pia ya Mungu kwamba msaada wa Mugnu uthibitike kwa maisha, heshima na mali yangu, yaani kwa njia zote tatu na kwa jiha zote tatu. Kwani, kuhusu uhai na heshima, msaada wa Mungu ulikwishathibitika katika kesi ya Dr. Martin Clark; lakini msaada wa Mungu kuhusiana na mali ulikuwa bado ulifichikana, basi fadhili na ukarimu wa Mwenyezi Mungu ukakusudia kuwaonyesha watu msaada wake unaohusu mali pia. Basi, kwa kuonyesha msaada huu pia akakamilisha duara la misaada ya aina zote tatu. Hivyo, hiyo ndiyo siri kwamba ikaanzishwa kesi hii. Kama vile kesi ya Dr. Clark haikuanzishwa mintarafu ya Mwenyezi Mungu ili niangamizwe au nidhalilishwe, bali ilianzishwa ili bishara za Yule Mweza Mkarimu zidhihirike, ndivyo ilivyokuwa katika kesi hii pia. Na kama vile Mola wangu Alivyoishatoa bishara mapema katika kesi ya kuhusu uhai na mali yangu kuwa mwishoni nitaachiwa huru na maadui watadhalilika, ndivyo hivyo Alivyoishatoa katika kesi hii pia bishara ya habari njema kuwa mwishowe ushindi nitapata mimi na mahasidi waovu watashindwa. Na ile bishara ya kiufunuo ilikwisha pata kuenea ndani

ya Jumuiya yangu kabla ya uamuzi wa mwisho kutolewa. Na kama katika kesi ya uhai na heshima, Jumuiya yangu ilivyoshuhudia ishara moja ya kimbingu ndivyo walivyoona ishara moja ya kimbingu ambayo imekuwa ni sababu ya kuongezeka imani yao. Alhamdulillahi!

Nastaajabu sana kuwa ingawa ishara baada ya ishara zinaendelea kudhihirika, lakini hata hivyo masheikh hawaelekei kuukubali ukweli. Hawaoni kuwa katika kila medani Mwenyezi Mungu Anawafanya washindwe. Wanataka sana kuwa ithibitike kwamba wanasaidiwa na Mungu, lakini badala ya msaada yaendelea kuthibitika siku hadi siku kuachwa kwao bila msaada na kutokufanikiwa kupata utashi. Kwa Mfano, katika zile siku ilipoenea habari iliyoandikwa katika takwimu kwamba katika mwezi huu wa Ramadhani, jua na mwezi vyote viwili vitapatwa na watu wakapata kufikiria nyoyoni kuwa hii ndiyo alama ya kudhihiri Imamu aliyeahidiwa, hapo mioyo ya Masheikh ikaanza kudunda kuwa mdai wa kuwa Mahdi na Masihi ndiye mtu huyu tu mmoja aliyesimama uwanjani, isije watu wakaelekea kwake. Ndipo kwa kuficha alama hiyo, kwanza baadhi yao wakaanza kusema kuwa jua na mwezi kamwe havitapatwa ndani ya mwezi

huu wa Ramadhani, bali vitapatwa wakati atakapodhihiri Imam Mahdi wao, na vilipokwishapatwa mwezi na jua katika Ramadhani, basi wakaleta udhuru kuwa kupatwa huku kwa jua na mwezi hakukutokea sawa na maneno ya Hadithi, maana ndani ya Hadithi imeelezwa kuwa mwezi utapatwa katika usiku wa kwanza na jua litapatwa katika tarehe ya katikati, ambapo mwezi umepatwa katika usiku wa kumi na tatu na jua limepatwa tarehe ishirini na nane. Na walipofahamishwa kuwa Hadithi haimaanishi tarehe ya kwanza, kwani mwezi wa tarehe ya kwanza hauwezi kuitwa Qamar, bali waitwa hilali; na katika Hadithi neno Qamar limetumika sio Hilali. Basi, Hadithi yamaanisha kuwa mwezi utapatwa katika usiku wa kwanza katika siku zake za kupatwa, yaani, tarehe kumi na tatu ya mwezi; na jua litapatwa katika siku ya katikati yaani tarehe ishirini na nane ambayo ndiyo siku ya katikati ya siku zake za kupatwa[38].

---

[38] Hii ndiyo kanuni inayofanya kazi ulimwenguni kwamba kwa kupatwa mwenzi imepangwa siku tatu, yaani usiku wa tarehe kumi na tatu, kumi na nne na kumi na tano. Na daima mwezi hupatwa ndani ya usiku mmojawapo katika hizi tatu. Basi, sawa na hesabu hii usiku wa kwanza wa kupatwa mwezi ni tarehe 13, iliyoashiriwa katika Hadithi. Na siku za kupatwa

Ndipo Masheikh wasio na ujuzi wakafedheheka sana baada ya kuelezwa maana hii sahihi. Kisha kwa kujitahidi sana wakazua udhuru mwingine kuwa katika wasimulizi wa Hadithi hii msimulizi mmoja si mtu mzuri. Hapo wakaambiwa kwamba ikiwa bishara imekwishatimia, kukosoa huku ambako msingi wake ni shaka si chochote dhidi ya tukio hili la yakini ambalo ni dalili madhubuti juu ya ukweli wa Hadithi. Yaani kutimia kwa utabiri kunashuhudia kuwa haya ni maneno ya mkweli. Na kusema kuwa yeye si mkweli bali yu mwongo ni kukana hakika isiyokanika na wenye akili. Na daima kanuni ya muhadditхina ndiyo hii kwamba wanasema kuwa shaka haiwezi kuondoa yakini. Kutimia kwa bishara sawasawa na maana yake katika zama ya mdai wa umahdi ni ushahidi wa yakini juu ya jambo hili kwamba mwenye kutamka maneno haya amesema kweli. Lakini kusema kuwa tuna shaka kuhusu mienendo yake ni jambo ambalo lenyewe lina shaka; na pengine mwongo pia anasema kweli. Zaidi ya hayo, bishara hii inathibitika kwa njia nyingine pia. Baadhi ya wakuu wa dhehebu la Kihanafii pia

---

jua ni tarehe 27, 28 na 29 za mwezi. Basi, kwa hesabu hii siku ya katikati ya kupatwa kwa jua ni tarehe 28. Na katika tarehe hizo hizo jua na mwezi vilipatwa — Mwandishi.

wameiandika hiyo. Hivyo, basi kukataa siyo uadilifu, bali ni kichwa ngumu tu. Na baada ya kupata jibu la kunyamazisha, wakalazimika kusema kuwa Hadithi hii ni sahihi na kutokana na hii inaeleweka kuwa hivi karibuni Imamu aliyeahidiwa atadhihiri; lakini mtu huyu siye Imamu aliyeahidiwa, bali atakuwa mwingine ambaye baada yake hivi karibuni atadhihiri. Lakini jibu lao hili nalo likathibitika kuwa ni bovu na batili; kwani, kama pangelikuwepo Imamu mwingine ilimpasa huyo Imamu kuja mwanzoni mwa karne kama Hadithi inavyomaanisha. Lakini katika karne, imeishapita miaka kumi na mitano, na Imamu wao yeyote hajadhihiri. Sasa jibu kutoka kwao ni hili kuwa watu hawa ni makafiri, msisome vitabu vyao, msikutane nao, msisikilize maneno yao, maana maneno yao yanaathiri mioyoni. Lakini hapa pana onyo, kwani mbingu pia inawapinga na hali ya sasa ya ardhi pia inawapinga. Ni dhila yao kiasi gani kuwa upande mmoja mbingu inashuhudia dhidi yao na upande mwingine ardhi yashuhudia kutokana na itikadi ya Msalaba kupata nguvu. Ushahidi wa mbingu umo ndani ya kitabu cha Daar Qutni na vinginevyo, yaani kupatwa kwa jua na mwezi ndani ya mwezi wa Ramadhani. Ushahidi wa ardhi ni Ukristo

kupata nguvu ambapo Masihi Mau‘udi alilazimika aje, na Hadithi hii imo ndani ya Sahihi Bukhari. Shahada zote mbili hizi zinatuunga mkono na zinawakadhibisha. Kisha alama ya kifo cha Lekhram iliyodhihiri nayo imewafedhehesha vya kutosha. Kadhalika mkutano wa dini wa mataifa ambamo makala yangu ilishinda ikiwa kama ishara haukuwa aibu ndogo, kwani siyo tu kwamba makala yangu ilishinda bali mapema kwa kupata ufunuo habari hiyo ilienezwa kwa njia ya vipeperushi. Laiti kama Atham angeishi hapo Sheikh Muhammad Husain wa Batala na wenzake wangepata mwanya wa kutoa maelezo ya uongo kiasi fulani, lakini Atham naye akafa haraka na akawaangamiza jamaa hawa. Maadamu alikaa kimya akaishi, lakini alipofungua tu midomo sharti ya ufunuo ikamkamata. Mwenyezi Mungu Alimpa umri sawa na sharti iliyoelezwa katika ufunuo, na alipoanza kukadhibisha, kuanzia hapo magonjwa makali yakamshika na katika muda mfupi tu yakamaliza maisha yake. Lakini kwa kuwa baadhi ya masheikh wapumbavu hawakuihisi aibu hii, na bishara yenye sharti wakaiangalia kikorofi kana kwamba hakukuwepo sharti lolote, na kwa uadilifu hawakupata maarifa kutokana na kubumbuazwa kwa Atham na kukaa

kwake kimya katika muda wote wa utabiri, wala hawakupata mwongozo kwa mambo yote ambapo Atham akaitwa kwa kuapa na kushawishiwa kwenda kushtaki mahakamani akakataa kwa kushika masikio yake, hivyo Mungu Asiyetaka ishara zake zibakie za mashaka, Akatimiza waziwazi, kwa kukamilisha hoja, utabiri kumhusu Lekhram ambao hakuwa na sharti lolote lile, na ambamo tarehe, siku na jinsi atakavyokufa, vyote vilikuwa vimeelezwa. Lakini inasikitisha kuwa wapinzani wa ukweli hata hawakujifaidisha na ishara hii wazi wazi ya Mwenyezi Mungu. Ni dhahiri kuwa kama mimi ningekuwa mwongo, bishara kumhusu Lekhram ilikuwa nafasi nzuri ya kunidhalilisha mimi, kwani hakukuambatana na sharti lolote. Nami kwa uwazi kabisa nikatangaza ikrari kimaandishi kuwa bishara hii ikitokea kuwa ya uongo, basi mimi ni muongo na ninastahili kila aina ya adhabu na dhila. Hivyo basi, kama mimi ningekuwa mwongo, lazima Mwenyezi Mungu Angenidhalilisha, angefuta jina langu na la Jumuiya yangu. Kwa sababu utabiri huu ulitangazwa kwa kuapa ambao haukuwa na sharti lolote. Lakini Mungu hakufanya hivyo, bali kwa njia hiyo Akadhihirisha heshima yangu, na wale ambao kwa kutojua hawakuielewa vizuri bishara

ilivyomhusu Atham, Akatia mwangaza katika mioyo yao kwa bishara hii. Je, hapa siyo mahali pa kufikiria kuwa kwa nini Mungu Akanisaidia kuhusu utabiri ambao haukuwa na sharti lolote na ambao kubatilika kwake safina yangu yote ingeghariki, na kwa nini Akiutimiza Akatia mahaba yangu katika mamia ya mioyo, hata kwamba baadhi ya maadui wakali wakaja kufanya baiati huku wakilia? Kama bishara hii isingetimia, Sheikh Batalawii afikirie mwenyewe kuwa angejitahidi namna gani kuandika ndani ya gazeti lake la "Ishaatus Sunah" makala za kunikadhibisha, nazo zingeiathiri dunia namna gani! Je, mtu anaweza kufikiria kwa nini Mwenyezi Mungu Alimuaibisha na kumdhalilisha Batalawii na wenzake wenye mawazo yake katika wakati kama huu? Je, haimo ndani ya Kurani Tukufu kuwa Mungu Ameshaandika kuwa Yeye Huwashindisha waaminio? Je, bishara hii ambayo haikuwa na sharti hata kidogo na ilimhusu mpinzani mkubwa aliyekuwa ananisagia meno, kama ingebatilika, je, baada ya matokeo haya ya wazi ningebakiwa na heshima yoyote? Na je, siyo sahihi kuwa bishara hii ingelibatilika, sheikh Muhammad Husain Batalawii angelipata furaha ya idi elfu na angelijaza gazeti lake kebehi, cheko

za dharau, na angeitisha mikutano kadhaa. Lakini sasa baada ya bishara kutokea kuwa ya kweli yeye amefanya nini? Je, sio kweli kuwa ameitupa kama takataka kazi moja kubwa kabisa ya Mwenyezi Mungu, na akadokeza ndani ya gazeti lake lenye mkosi kuwa eti mwuaji wa Lekhramu ni mtu huyu huyu. Basi, ninasema kuwa mimi si mwuaji wake kwa kutumia silaha ya kibinadamu; naam, kwa kutumia silaha ya kimbinguni, yaani kwa njia ya kuomba dua mimi ni mwuaji, na hiyo pia baada ya yeye kung'ang'ania na kuniomba sana. Sikupenda kumwombea vibaya, lakini yeye mwenyewe akataka hivyo. Hivyo, mimi ni mwuaji wake jinsi Nabii wetu[saw] alivyokuwa mwuaji wa Mfalme wa Irani Khusro Parvez. Ilmuradi, kesi ya Lekhramu ikatimiza hoja ya Mwenyezi Mungu juu ya Muhammad Husain na kadhalika juu ya ndugu zake wengine.

Kisha baada ya hapo ikadhihirika ishara ya Mungu katika kesi ya Daktari Clark, na ule utabiri ukatimia uliokuwa umekwisha enea baina ya mamia ya watu kabla ya hukumu ya mwisho. Katika kesi hiyo Sheikh Batalawii alipata kufedheheka sana, na kama bahati njema ingelimsaidia wema bila shaka angelifanya toba halisi bila kuchelewa. Imekwisha bainika kwake

kuwa Mungu Alimsaidia nani?

Ikumbukwe kuwa katika kesi ya Dr. Clark, Mohammad Husain akiungana na Wakristo, alitumia nguvu zake zote kuniangamiza wala hakuachia nafasi hata kidogo ya kunidhalilisha. Mwishoni Mola wangu Akaniachia huru. Na yeye alipoomba kiti cha kukalia ndani ya mahakama hasa akapata fedheha ambayo mtu mwungwana anaweza kujifia kwa kuaibika hivyo. Haya ni matokeo ya kumtakia fedheha mtu wa haki. Alipoomba kiti, mheshimiwa mkuu wa wilaya akamgombeza Batalawii na kumwambia hujawahi kupewa kiti hapa wala baba yako; na kwa kumkaripia akamsukumia nyuma na akamwambia simama wima. Na msiba juu ya msiba ni kwamba alipokuwa akikaripiwa, mimi — ambaye sheikh huyo alikuja kushuhudia fedheha yangu — nilikuwa nimekaa kitini karibu na mheshimiwa Mkuu wa Wilaya. Mimi sina haja ya kuirudia-rudia; maofisa wa mahakama wapo na wafanyakazi wao nao wapo; anayetaka kuwauliza na awaulize.

Sasa hapa swali lenyewe ni hili kuwa kuna ahadi ya Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu kuwa yeye Huwasaidia waaminio na kuwapa heshima; na Anawadhalilisha waongo na

madajali. Sasa mambo yamepindukaje hata kwamba katika kila uwanja Muhammad Husain ndiye aliyeendelea kudhalilika na kufedheheka na kuvunjiwa heshima? Je, hii ndiyo desturi ya Mwenyezi Mungu kwa wapendwa wake? Sasa, katika kesi ya kodi, furaha ya Sheikh Batalawii ilikuwa kwamba kwa vyovyote vile nitozwe kodi ya mapato ili kwa kuikuza na kuipanua habari hii alipambe gazeti lake la “Ishaatus Sunnah”, ili fedheha alizozipata hapo kabla ziweze kufunikwa kiasi fulani. Lakini katika hiyo pia ameshindwa, kwani hukumu bayana ya kusamehewa kodi ikaja. Mungu Aliiweka kesi hii mikononi mwa mahakimu waliotimiza wajibu wa uadilifu kwa ukweli na uaminifu. Basi, wakorofi wenye bahati mbaya wakashindwa katika shambulio hili. Maelfu ya shukrani ni kwa Mwenyezi Mungu Ambaye Aliwabainishia mahakimu waadilifu uhakika hasa. Na hapa napaswa kumshukuru Mheshimiwa T. Dixon, Makamu wa Kamishna wa Wilaya ya Gurdaspur ambaye Mwenyezi Mungu Alimfichulia ukweli ulivyo. Ndiyo maana mimi tangu mwanzo naishukuru dola ya Kiingereza na mahakimu wa Kiingereza na ninawasifu, kwani kwa vyovyote wanautanguliza uadilifu. Mheshimiwa Kapteni Douglas, Kamishna wa

zamani, katika kesi ya Daktari Clark, na Bwana T. Dixon katika kesi ya kodi ya mapato wametuonyesha mifano miwili ya kupenda uadilifu na haki ambayo hatuwezi kusahau maisha yote. Kwani, mbele ya Kapteni Douglas kulikuwa na kesi nyeti sana ambayo mdai wake alikuwa ni Mkristo mmoja mwenye heshima ambaye kana kwamba aliungwa mkono na mapadri wote wa Punjab, lakini hakimu huyu hakujali kitu kuwa kesi ile ilifunguliwa na kundi gani, bali akafanya uadilifu barabara na akatoa hukumu kwamba sina hatia. Na kesi ambayo sasa ilifikishwa katika mahakama ya Bwana T. Dixon, hiyo pia ilikuwa nyeti, maana kusamehe kodi ya mapato ni hasara kwa serikali. Basi, mheshimiwa huyu naye akafanya haki na uadilifu kabisa. Nifikirivyo, mahakimu wa aina hii ndio mifano ing'aayo ya kuwalinda raia, nia njema na uadilifu. Na hakika yenyewe ndiyo hiyo ambayo busara ya Bwana T. Dixon iliitambua. Hivyo, nashukuru na ninaomba pia dua. Na hapa panastahili kutajwa juhudi na utafiti wa Munshi Tajuddin, Mkuu wa tarafa ya Batala ambaye kwa kukusudia uadilifu na kuhakikisha haki akawaonyesha mahakimu wenye madaraka matukio ya kweli kama kioo, na kwa njia hii akawasaidia wenye madaraka ya juu

kufikia uhakika ulivyo. Sasa hapa chini yaandikwa kesi hiyo, yaani maoni ya mkuu wa Tarafa na hukumu ya Makamu wa Kamishna kuhusu kesi hii inaandikwa chini:

Nakala ya taarifa ya Munshi Tajuddin, Mkuu wa Tarafa, tarafa ya Batala, wilaya ya Gurdaspur, kuhusu kesi ya pingamizi la kutozwa kodi ilivyomo katika faili ya kikao cha Bwana T. Dixon Makamu wa Kamishna, iliyorejewa 27 Juni 1898, uamuzi ulitolewa 17 Septemba 1898, namba ya usajili ya mahakama, namba ya kesi 55/46, faili ya kukinza kutozwa kodi ya mapato ya Mirza Ghulam Ahmad bin Ghulam Murtaza, ukoo Mughali, mkazi wa Qadian,

Tarafa ya Batala, wilaya ya Gurdaspur.

Mkuu wa wilaya ya Gurdaspur.

Kwa Mheshimiwa Mkuu wa wilaya ya Gurdaspur,

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian alikadiriwa alipe mwaka huu kodi ya mapato Rupia 187 Anna 8. Kabla ya hapo Mirza Ghulam Ahmad hakukadiriwa kulipa kodi. Kwa vile kodi hii ni mpya, Mirza Ghulam Ahmad ameleta mahakamani mwako ombi la udhuru lililoletwa katika ofisi hii kwa kupelelezwa. Kabla ya kueleza uchunguzi uliofanywa kuhusu kodi ya

mapato, yafaa kukuelezea machache kumhusu Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian ili ijulikane kuwa mpingaji ni nani na ni mtu wa daraja gani.

Mirza Ghulam Ahmad anatokana na ukoo mmoja wenye heshima wa zamani wa Mughali, anayeishi kijijini Qadian kwa muda mrefu. Baba yake Mirza Ghulam Murtaza alikuwa mmliki wa ardhi nyingi, mwenye heshima, na alikuwa chifu wa Qadian. Yeye alipofariki akaacha milki nyingi ambayo sehemu fulani ya milki hiyo anayo Mirza Ghulam Ahmad mpaka sasa, na sehemu fulani anayo Mirza Sultan Ahamd mwanaye Mirza Ghulam Ahmad aliyopata kupitia mjane wa marehemu Mirza Ghulam Qadir. Sehemu kubwa ya milki hii ni ardhi ya kilimo kama vile bustani, mashamba na vijiji vichache. Na kwa vile Mirza Ghulam Murtaza alikuwa chifu mwenye heshima kubwa, inawezekana, bali katika rai yangu yawezekana sana, kuwa aliacha pesa nyingi taslimu na mapambo mengi ya dhahabu pia, lakini kuhusu mali isiyohamishika hakuna ushahidi wa kuridhisha. Katika siku za awali, Mirza Ghulam Ahmad mwenyewe alikuwa anafanya kazi, na jinsi ulivyo mwenendo wake siku zote haiwezi kufikiriwa kama akaangamiza mapato yake au mali ya baba yake, pesa taslimu na mapambo ya

dhahabu. Mali isiyohamishika aliyorithi kwa baba yake ipo mpaka sasa, lakini kuhusu mali inayohamishika ushahidi wa kutosha haukupatikana. Lakini kwa vyovyote, sawa na hali ya Mirza Ghulam Ahmad inaweza kusemwa kwa yakini kabisa kuwa mali hiyo pia hakuiangamiza. Tangu muda fulani Mirza Ghulam Ahmad ameacha shughuli zote za kazi na amejielekeza kwenye dini yake. Na sikuzote akajaribu akubaliwe kuwa kiongozi wa dini. Yeye akaandika vitabu vichache vya dini, akaandika vijitabu, na kwa njia ya matangazo akaeleza fikara zake. Matokeo ya shughuli zote hizi ni kuwa tangu muda fulani kundi la watu wengi, ambao orodha yao (katika herufi za Kiingereza) imeambatanishwa na taarifa hii, likaanza kumtambua kuwa yeye ni kiongozi wao, hivyo likaimarika kama dhehebu la kujitegemea. Sawa na orodha inayoambatanishwa hapa, hivi sasa dhehebu hili lina watu 318 ambao miongoni mwao wamo — japo si wengi — baadhi ya watu wenye heshima na utaalamu. Kundi la Mirza Ghulam Ahmad lilipopanuka na kuongezeka hapo Mirza Ghulam Ahmad akawahimiza wafuasi wake ndani ya kitabu chake ‘Fat-he Islam’ na ‘Taudhihe Maram’ kutoa mchango kwa kutimiza shabaha

zake, na kwa kufikia shabaha iliyokusudiwa akaelekeza wafuasi wake kutoa michango. Akaeleza mambo matano yanayohitaji michango. Kwa vile wafuasi wa Mirza Ghulam Ahmad wakawa na imani naye, hivyo polepole wakaanza kumpelekea michango, na katika barua zao pengine wakaeleza kwamba mchango wao ndio kwa jambo fulani maalumu katika mambo hayo matano, na pengine wakamwachia Mirza Ghulam Ahmad autumie katika jambo lolote miongoni mwa mambo hayo matano analoonelea linahitaji. Na ndivyo zinavyotumika fedha za mchango sawa na maelezo ya Mirza Ghulam Ahmad na sawa na ushahidi wa mashahidi. Ilmuradi, kundi hili hivi sasa ni jamii ya kidini ambayo Mirza Ghulam Ahmad ndiye kiongozi wake, na wengine wote ni wafuasi na wanatimiza malengo ya jamii yao kwa kutoa mchango. Mambo matano yaliyoelezwa hapo juu ni haya yafuatayo:

1. Nyumba ya Wageni: Watu wote wanaokuja Qadian kwa Mirza Ghulam Ahmad, wakiwa wafuasi au wasiokuwa wafuasi, lakini wawe wamekuja kwa ajili ya utafiti wa kidini wapata chakula kutoka hapo. Na sawa na maelezo ya kimaandishi ya mwakilishi wa Mirza Ghulam Ahmad michango ya sehemu hii wanasaidiwa

wasafiri, mayatima na wajane pia kutoka katika mchango wa mfuko huu.

2. Kiwanda cha Uchapaji: Vitabu vya kidini, na matangazo huchapwa na pengine watu wanagawiwa bure.

3. Madrasa: Wafuasi wa Mirza Ghulam Ahmad wameanzisha madrasa moja ambayo hivi sasa ipo katika hatua za mwanzo, inayosimamiwa na Maulawii Nuruddin ambaye ni mfuasi mahsusi wa Mirza Ghulam Ahmad.

4. Mkutano wa Mwaka na mikutano mingine: Kundi hili linafanya pia mikutano ya mwaka, na kwa maandalio ya mikutano hiyo mchango unachangwa.

5. Kuandika barua: Kutokana na maelezo ya kimaandishi ya mwakilishi wa Mirza Ghulam Ahmad na kwa ushahidi wa mashahidi, fedha nyingi zinatumika katika shughuli hii. Barua zote zinazoandikwa kuhusu utafiti wa kidini zinalipwa kutokana na mchango wa wafuasi. Ilmuradi, sawa na maelezo ya mashahidi, mchango huu wote hutumika katika mambo haya matano, na kwa njia hizi Mirza Ghulam Ahmad anaeneza fikara zake za dini na za wafuasi wake. Jamii hii ni kundi la kidini, na kwa kuwa mheshimiwa unalijua

mapema kundi hili, hivyo maelezo haya mafupi yanatosha. Na sasa natoa maelezo kuhusu ombi lenyewe la kuondolewa kodi.

Mapato ya mwaka ya Mirza Ghulam Ahmad yakakadiriwa Rupia 7, 200 kwa mwaka huu, na ikakadiriwa atoe kodi ya mapato Rupia 187 Anna 8. Alipopinga kutozwa huku nilichukua maelezo yake hasa kijijini Qadian nilipokwenda huko katika matembezi yangu na ushahidi wa mashahidi kumi na watatu uliandikwa. Mirza Ghulam Ahmad aliandikisha maelezo yake kwa kiapo kuwa mapato yake yanatokana na mashamba, ardhi na bustani. Mapato kutoka mashamba kwa mwaka ni Rupia 83 Anna 10 takriban, na kutoka ardhi ni karibu Rupia 300 kila mwaka, na mapato kutoka bustani ni karibu rupia mia mbili, mia tatu, mia nne hadi mia tano; zaidi ya hayo hana mapato yoyote. Mirza Ghulam Ahmad akaeleza pia kuwa mwaka huu amepata Rupia 5,000 kutoka kwa wafuasi wake, waila kila mwaka kwa wastani anapata karibu Rupia 4,000 ambazo zinatumika katika mambo matano yaliyotajwa hapo juu, na hatumii kwa haja zake binafsi. Hesabu ya mapato na matumizi haikuwekwa kikawaida, bali ameandikisha kutokana na kumbukumbu. Mirza Ghulam Ahmad

pia alieleza kuwa mapato yake bianfsi yanayotokana na bustani, ardhi na shamba yanatosha kwa ajili ya matumizi yake mwenyewe; hana haja ya kutumia fedha za wafuasi wake kwa matumizi yake binafsi. Ushahidi wa mashahidi pia unaafikiana na maelezo ya Mirza Ghulam Ahmad. Na inaelezwa kuwa wafuasi wanamtumia fedha Mirza Ghulam Ahmad kwa ufadhili ili kutekelezea mambo hayo matano, nazo zatumika kwa mambo hayo hayo. Mirza Ghulam Ahmad hana mapato yake ya binafsi mbali na mapato yake yanayotokana na shamba, ardhi na bustani yanayoweza kutozwa kodi. Miongoni mwa mashahidi kuna mashahidi sita ambao ingawa wanaaminika sana, lakini ni wafuasi wa Mirza Ghulam Ahmad, na wakati mwingi wanakaa pamoja naye. Mashahidi wengine saba ni wenye maduka wa namna mbalimbali ambao hawana uhusiano wowote na Bwan Mirza. Kwa ujumla, mashahidi wote hawa wanaafikiana na maelezo ya Mirza Ghulam Ahmad na wanasema kwamba hana mapato yake binafsi mbali na mapato yatokanayo na mashamba, ardhi na bustani. Mimi niliwauliza baadhi ya watu kwa siri kuhusu mapato ya binafsi ya Mirza Ghulam Ahmad. Ingawa nilielezwa na baadhi ya watu kuwa

mapato ya Mirza Ghulam Ahmad ni makubwa na yanatakiwa kutozwa kodi, lakini sikupata uthibitsho bayana wa mapato ya Bwana Mirza. Ikasemwa tu kwa midomo lakini mtu yeyote hakuweza kuthibitisha kikamilifu. Mimi hapo Qadian nikajionea mwenyewe nyumba ya wageni, madrasa pia. Madrasa bado ipo katika hatua ya mwanzo na majengo yake zaidi ni ya udongo, kuna nyumba chache pia kwa wafuasi wake, lakini kwenye nyumba ya wageni walikuwepo wageni na nikaona pia kwamba wageni wote waliokuwepo siku hiyo walikula chakula katika nyumba hiyo ya wageni.

Maoni yangu mimi ni kwamba kama mapato ya Mirza Ghulam Ahmad yachukuliwe kuwa yanatokana na mashamba na bustani kama inavyobainika kutokana na ushahidi, na mapato anayopata kutoka kwa wafuasi wake yachukuliwe kuwa ni fedha za sadaka kama mashahidi walivyoelezea, hapo Mirza Ghulam Ahmad hawezi kudaiwa kulipa kodi ya mapato. Lakini inapofikiriwa upande wa pili kuwa Mirza Ghulam Ahmad anatokana na ukoo mkubwa sana wenye heshima, na wazazi wake wamewahi kuwa machifu na mapato yao yalikuwa makubwa, na Mirza Ghulam Ahmad mwenyewe aliwahi

kufanya kazi na alikuwa mwenye hali nzuri, hapo lazima inadhaniwa kuwa Mirza Ghulam Ahmad ni mtu tajiri naye anastahili kutozwa kodi ya mapato. Sawa na maelezo ya Bwana Mirza mwenyewe hivi karibuni aliweka rehani bustani lake kwa mkewe na akapata mapambo ya dhahabu ya Rupia elfu nne, na Rupia elfu moja taslimu toka kwake. Basi, mtu ambaye mkewe anaweza kutoa kiasi hicho cha fedha kumhusu yeye lazima yadhaniwa kwamba mtu huyo ndiye tajiri. Uchunguzi nilioufanya umetiwa ndani ya faili, na sawa na agizo lako nakuletea taarifa hii iliyoandikwa tarehe 31 Agosti 1898.

Mnyenyekevu Tajuddin

Mkuu wa tarafa ya Batala

Taarifa ya ziada: Mwakilishi wa Mirza Ghulam Ahmad ameagizwa kuhudhuria mahakamani mwako tarehe 3 Septemba 1898. —Tarehe ya maandishi: iliyotajwa juu.

Saini ya Hakimu

Nakala ya hukumu ya muda iliyotolewa katika mahakama ya Bwana T. Dixon Makamu wa Kamishna wa Gurdaspur, kuhusu pingamizi la kutozwa kodi.

Faili ya pingamizi la kutozwa kodi ya mapato ya Mirza Ghulam Ahmad bin Ghulam Murtaza, ukoo Mughal, mkazi wa Qadian, tarafa ya Batala, wilaya ya Gurdaspur.

Taarifa hii ya Mkuu wa Tarafa imetolewa na kusikilizwa leo. Kwa hivi sasa ni kwamba faili hii iwe inafikiriwa. Sheikh Ali Ahmad, wakili na mwakilishi wa mkinzani, yupo hapa na yeye amearifiwa.

Saini ya Hakim, Tarehe: 03.09.1898

Nakala ya tafsir ya hukumu ya mwisho kuhusu pingamizi la kutozwa kodi ya mapato, iliyotolewa katika mahakama ya Bwana T. Dixon Makamu wa kamishna, wilaya ya Gurdaspur.

## Tafsiri ya Hukumu

Kodi hii iliyokadiriwa ni mpya na Mirza Ghulam Ahmad anadai kuwa mapato yake yote haya hayatumiki kwa ajili ya shughuli zake binafsi, bali hutumika kwa ajili ya mahitaji ya Jumuiya yake aliyoianzisha. Anakubali kuwa ana mali nyingine pia, lakini alitoa taarifa mbele ya Mkuu wa Tarafa kuwa mapato yanayotokana na ardhi na kilimo na hayatozwi kodi chini ya kifungu cha sheria 5 (b) yanatumika kwa shughuli za dini. Sioni sababu ya kumtilia shaka nia yake njema, nami naondolea

mbali kodi ya mapato yake kutokana na michango, ambayo ameeleza kuwa ndiyo Rupia 5200/=, kwani chini ya kifungu 5 (c) cha sheria, hayo yatumika kwa ajili ya shughuli za dini tu. Hivyo hukumu inatolewa kuwa baada ya kutimiza kawaida karatasi hizi zitunzwe ofisini.

Saini ya hakimu, 17.09.1898, mjini Dalhousie.

Hapa chini tunanakili matini ya amri yenyewe ya mwisho katika lugha ya Kiingereza na tafsiri yake pia:

In the Court of F.T. Dixon Esquire Collector of the District of Gurdaspur.

Income Tax objection case No. 46 of 1898.

Mirza Ghulam Ahmad son of Mirza Ghulam Murtaza, caste Mughal, resident of mauza Qadian Mughlan, Tahsil Batala, Distt. of Gurdaspur, objector.

## ORDER

This tax is a newly imposed one and Mirza Ghulam Ahmad claims that all his income is applied not to his personal but to the expenses of sect he has founded. He admits that he has other property but he stated to the Tahsildar that even the proceeds of that which is classed as land and

the proceeds of agriculture and is exempt under 5 (b) go to his religious expenses. I see no reason to doubt the bona fides of this man, whose sect is well known, and I exempt his income from subscriptions which he states as 5200/- under Sec 5 (c) as being solely employed in religious purposes.

Sd/T. Dixo Collector

17-9-1898

## Tafsiri

Katika Mahakama ya Bwana F. T. Dixon, Mtoza kodi, Wilaya ya Gurdaspur.

Kesi Na. 46 ya mwaka 98 ya pingamizi la kutozwa kodi ya mapato.

Mpingaji: Bwana Mirza Ghulam Ahmad bin Mirza Ghulam Murtaza wa kabila la Mughal, mkazi wa Qadian, Tarafa ya Batala, Wilaya ya Gurdaspur.

## Uamuzi

Kodi hii iliyotozwa ni mpya. Mirza Ghulam Ahmad anaeleza kuwa mapato haya yote hutumika kwa ajili ya Jumuiya yake, hayatumiki kwa ajili yake binafsi. Yeye anakubali jambo hili

pia kuwa ana mali nyingine vilevile. Lakini ameeleza mbele ya Mkuu wa Tarafa kuwa hata mapato ambayo inatokana na ardhi na mazao na kilimo na hayatozwi kodi chini ya kifungu cha 5(b), yanatumika kwa mahitaji ya dini. Sioni sababu ya kutilia shaka nia yake, ambaye Jumuiya yake inajulikana kwa kila mtu. Ninaondolea mbali kodi ya mapatao ya michango yake — anayoeleza ndiyo Rupia 5200 na yanatumika kwa ajili ya mambo ya dini tu — chini ya kifungu cha 5(c) cha sheria.

Saini ya Bwana T. Dixon, Mtoza kodi.
17 Septemba 1898